

Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima (MKMEUWAWA)

Seti ya Zana za Utekelezaji

Awamu ya Tano – Pitia, Rekebisha na Panua Wigo



With financial support from the



Federal Ministry
for Economic Cooperation
and Development

Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUAWA)

Seti ya Zana za Utekelezaji

Kimechapishwa na:

Institute for International Cooperation of the German
Adult Education Association
(DfV International)
Königswinterer Straße 552b
53227 Bonn
Germany

Simu. +49 (0) 228 97569-0
Nukushi. +49 (0) 228 97569-55
info@dfv-international.de
www.dfv-international.de
© DfV International 2020
(Toleo la Kwanza)

Mwandishi & Mbunifu/Mwendeleza Mkabala:

Sonja Belete

Mwajibikaji/Mhariri Mtendaji:

Uwe Gartenschlaeger

Wasaidizi wa Utafiti:

Penny Ward (Mutengo Consulting),
Prof. Heribert Hinzen

Uhakiki/Uhariri wa Kiingereza:

Penny Ward (Mutengo Consulting)

Michoro:


Zerihun Gebrewold Lemma

Upangaji/Usanifu:

Gastdesign.de

Wafasiri wa Lugha ya Kiswahili:

Dkt. Sempeho I. Sifau, Scholastica Kileo, Chiraka
Muhura na Eric Samba **(Taasisi ya Elimu ya Watu
Wazima)**
Prof. Eustella Bhalalusesa, Dkt. Philipo Sanga na Dkt.
Leonard Bakize **(Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)**



Yaliyomo.....	3
Shukurani.....	4
Dibaji.....	5
Vifupisho.....	6
AWAMU YA TANO – PITIA, REKEBISHA NA PANUA WIGO.....	7
1. Utangulizi.....	8
2. Tafakuri kuhusu safari ya MKMEUWAWA: ujumbe muhimu na mada zinazojirudia.....	10
3. Muhtasari wa awamu ya upitiaji, marekebisho na upanuzi.....	13
4. Kupitia matokeo ya awamu ya kwanza hadi nne.....	15
4.1 Utangulizi wa mchakato wa upitiaji.....	15
4.2. Kusanifu mchakato wa upitiaji.....	17
4.2.1 Hatua katika kusanifu na kutekeleza upitiaji.....	17
4.2.2 Kujibu maswali muhimu kuhusu upitiaji.....	18
4.2.3 Kufanya upitiaji wa upande wa mahitaji ya huduma.....	22
4.2.4 Kupitia upande wa utoaji huduma za EUWAWA.....	24
4.2.5 Kuupitia ubia wa EUWAWA.....	25
4.2.6 Kuupitia mchakato wa MKMEUWAWA.....	27
4.3 Chambua na kukusanya matokeo ya upitiaji.....	28
5. Kufanya marekebisho ya lazima ili kujiandaa kwa upanuzi.....	30
5.1 Utangulizi wa mchakato wa marekebisho.....	30
5.2 Marekebisho katika utaratibu wa utoaji huduma za EUWAWA.....	33
5.3 Marekebisho katika ufanyaji kazi wa mfumo wa EUWAWA.....	35
5.4 Marekebisho katika ubia.....	39
5.5 Mpango wa kuyatendea kazi marekebisho katika mfumo wa EUWAWA na utoaji huduma.....	40
6. Panua wigo wa mfumo ulioboreshwa.....	42
6.1 Utangulizi wa mchakato wa kupanua wigo.....	42
6.2 Masuala yanayoathiri mchakato wa kupanua wigo.....	43
6.3 Mazingatio na hatua katika upanuzi.....	45
Uchanganuzi kifani wa Uganda.....	49
7. Hitimisho na hatua zinazofuat.....	52
Faharasa.....	53
Marejeleo.....	54



Uchapishaji wa seti ya zana hii na mfululizo kuandaa vitabu hivi, usingeweza kukamilika bila ya ushiriki wa karibu wa wafanyakazi wa shirika la DVV International katika ofisi za nchini Ethiopia na Uganda. Walitumia muda wao mwingi kusoma, kujadili, kupima, kutafakari na kutoa maoni na mawazo mpaka kile kilichoanza kama mfululizo wa warsha kadhaa kilipoibua mkabala madhubuti unaotoa mwelekeo wa kazi za DVV International katika kanda ya Mashariki/Pembe ya Afrika na zaidi ya hapo. Mwandishi angependa kutoa shukurani kwa Eshetu Abate, Amanuel Hedera na Caesar Kyebakola.

Washirika wa DVV International katika kanda, yaani Wizara ya Elimu (WyE) nchini Ethiopia na Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii (WJKMJ) nchini Uganda, wamekuwa mstari wa mbele katika kuthamini uwezo mkubwa wa mkabala huo hata katika hatua zake za awali.

Kwa ushirikiano na ngazi ya serikali za mitaa na ofisi nyingine ambazo zilishiriki warsha za mafunzo na tafakari, walifanya upitiaji taalimu, walichangia mawazo, na kupima seti ya zana, nadharia pamoja na awamu za mkabala huu. Wanaendelea kuutumia mkabala huu katika kazi zao za kila siku ili kujenga Mifumo Bora ya Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima.

Shukurani maalumu ziwaendee timu mbili zilizofanya upitiaji taalimu kuhusu Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima nchini Ethiopia katika ngazi zote za utekelezaji. Rejea maalumu inafanywa kwa:

- Timu iliyofanya tathimini kwa upande wa Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima (EUWAWA) na utoaji wa huduma ya EUWAWA mwaka 2018. Timu hii ya upitiaji taalimu haikutoa tu taarifa nyingi za msingi kuhusu mfumo huu nchini Ethiopia, bali pia kuzifanyia majaribio zana za Awamu ya Pili katika Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima (MKMEUWAWA).

- Timu iliyofanya tathimini ya upande wa wapokea huduma kuhusu mahitaji na maslahi ya wanafunzi wa EUWAWA kwa mwaka 2019/2020. Matokeo ya utafiti yalitoa msingi kwa uchambuzi zaidi wa Awamu ya Pili na kusaidia uandaji wa Awamu ya Tatu.

- Wafanyakazi wa makao makuu ya DVV International walioona umuhimu wa mkabala huu na kuwekeza muda wao mwingi katika kusoma na kutoa maoni yao. Bila msaada wao na kutoa kipaumbele katika kuboresha kazi hii, uandaji wa seti ya zana hii usingekamilika. Neno la shukurani kwa wafuatao;
- Naibu Mkurugenzi, Uwe Gartenschlager, ambaye alisimamia maandalizi ya seti ya zana hii na kutoa mwongozo, mchango, maoni na muda mwingi katika mchakato mzima. Msaada wake ulikuwa wa thamani sana.
- Mkurugenzi mtendaji Christoph Jost, kwa kutoa fursa ya kuandaa na kuchapisha seti ya zana hii.
- Frauke Heinze, Gerhard Quincke na Esther Hirsch kwa kukubali na kuendeleza zaidi mkabala huu.
- Wafanyakazi wote wa DVV International katika kanda ya Afrika kwa kuthibitisha na kukijaribu kiunzi cha dhana, awamu na zana za EUWAWA.

Zaidi ya hayo, ningependa kuwashukuru washiriki yaani Prof. Heribert Hinzen, kwa msaada wa tafiti na mchango kuhusu misingi ya kinadharia ya mkabala huu; Penny Ward kwa kufafanua zana ili kuwezesha michakato na uhariri wa lugha ya Kiingereza; Zerihun Gebrewold aliyeboresha kwa kupunguza maandishi kwa vielelezo vya rangi; Houssein Bel Hadj kwa tafsiri ya Kifaransa na GASTDESIGN kwa mpangilio na usanifu wa picha na watafasiri wote katika lugha zingine zilizosalia kazi yenu ya kitaalamu na bora sana ilisaidia seti hii ya zana kukamilika.

Sonja Belete



Wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipolitisha Malengo ya Maendeleo Endelevu

mwaka 2015, kilikuwa ni kipindi cha shangwe katika sekta ya elimu. Kwa mara ya kwanza Jumuiya ya Kimataifa ilikubali kwamba kujifunza ni maisha yote na fursa za kutosha za kujifunza zinapaswa kutolewa kwa watu wa rika, jinsi, jamii na makabila yote. Maendeleo haya yameleta matumaini kwamba wafanya uamuzi na wadau wakuu watapanua sera za elimu, na kuweka msisitizo mkubwa katika Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima (EUWAWA). Hata hivyo, japo ni dhahiri kwamba maboresho kadhaa yamefanyika, EUWAWA ndiyo sekta ndogo iliyopuuzwa zaidi katika mifumo mingi ya elimu ya kitaifa.

Changamoto kubwa inayozikabili taasisi nyingi za serikali na zisizo za serikali za elimu ya watu wazima, ni ukosefu wa mfumo wa kuendeleza, kufadhili, kufuatilia na kusaidia elimu na ujifunzaji kwa watu wazima (EUWAWA) katika ngazi ya taifa, kanda na ngazi za chini. Wakati nchi nyingi zikiwa na mifumo thabiti kwa ajili ya shule za msingi na sekondari, elimu ya juu na wakati mwingine elimu ya ufundi stadi, hali sivyo ilivyo kwa upande wa EUWAWA. Shirikia la Kimataifa la DVV lina uzoefu wa zaidi ya miaka 50 katika kusaidia uanzishwaji na uboreshaji wa mifumo ya EUWAWA. Somo moja tulilojifunza linalotokana na juhudi hizi ni kwamba hatua za pekepeke zina hatari kubwa ya kushindwa. Ndivyo ilivyo kwa michakato ambayo inategemea zaidi utaalumu wa kigeni na mifumo ya kuiga.

Kwa kuzingatia utangulizi huu, timu ya kimataifa ya DVV ya Mashariki au Pembe ya Afrika chini ya uongozi wa Sonja Belete ilianza mchakato wa kutengeneza modeli kamili ya uboreshaji endelevu wa mifumo ya EUWAWA. Vitabu hivi vinawasilisha

mbinu na uzoefu ambavyo viliandaliwa kwa muda mrefu. Ambao tunaita Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima (MKMEUWAWA) na umejikita katika uhalisia kadhaa;

- Ujenzi wa mfumo endelevu unatumia muda mwingi, mchakato wa muda mrefu ambao unahitaji uvumilivu na unyumbufu mkubwa.
- Umiliki ndiyo ufunguo. Wadau wa ndani wanapaswa kuunda mchakato na kutengeneza mfumo. Utaalamu wa nje unaweza kuwa na manufaa lakini haupaswi kuongoza mchakato au kulazimisha masuluhisho.
- Ujenzi wa mfumo unahitaji kujenga makubaliano kati ya washirika muhimu. Kigezo hiki ni muhimu kwa mafanikio hivyo kinapaswa kuwekwa tangu mwanzo na kiendeleo kutumika katika mchakato wote.

Sonja Balet na wenzake walibuni MKMEUWAWA kwa utaratibu wa kuanzia chini kwenda juu hasa kutokana na uzoefu wa nchi za Ethiopia na Uganda. Wakati huohuo, mkabala huo pia imetumiwa na nchi nyingine kumi barani Afrika. Mchakato huo umeboreshwa kwa kuzingatia kanuni za kujifunza kwa vitendo ili kuhakikisha kwamba miundo na zana zimeandaliwa na kuboreshwa zaidi wakati wa mchakato huu. Kujifunza kwa vitendo ni kigezo muhimu cha mafanikio ya mkabala huu na kinapaswa kutumika wakati wa utekelezaji wa mchakato. MKMEUWAWA ni mkabala ambao unaweza kuwaongoza wadau katika kazi ngumu ya kujenga mifumo, na wakati huohuo unaruhusu maboresho, ulinganisho na mabadiliko.

Tunakutakia mafanikio makubwa katika kujenga na kurekebisha mifumo ya Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima, na tunatumaini uzoefu wetu unaweza kuchangia kuboresha kazi yenu.

Uwe Gartenschlaeger

AZAJA.....	Asasi za Jamii
AZAKI.....	Asasi za Kiraia
AZISE.....	Asasi Zisizo za Serikali
DVV.....	Deutscher Volkshochschul-Verband
ECWW.....	Elimu Changamani ya Watu Wazima
EMAU.....	Elimu na Mafunzo ya Ufundi
EUWAWA.....	Elimu na Ujifunzaji kwa Watu Wazima
KIWAACHEMA.....	Kisomo cha Watu Wazima Chenye Manufaa
VJK.....	Vituo vya Jamii vya Kujifunzia
MAMV.....	Mipango ya Akiba na Mikopo Vijijini
MKKV.....	Mpango wa Kuweka na Kukopa Vijijini
MKMEUWAWA.....	Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima
MUT.....	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa
U&T.....	Ufuatiliaji na Tathmini Shirikishi
U&TS.....	Ufuatiliaji na Tathmini Shirikishi
UCHAJAKUU.....	Ujifunzaji Changamani wa Jamii wa Kuzalisha Utajiri
UJJKM.....	Ujifunzaji Jumuishi wa Jamii wa Kuzalisha Mali
UNDP.....	United Nations Development Programme
UNESCO.....	United Nations Education Scientific and Cultural Organisation
UNICEF.....	United Nations Children's Fund
VEWW.....	Vituo vya Elimu ya Watu Wazima
WJKMJ.....	Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii
WJKMU.....	Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Ujuzi

AWAMU YA TANO - PITIA, REKEBISHA NA PANUA WIGO


1. UTANGULIZI

Awamu ya Tano ya MKMEUWAWA inasogeza mbele lengo na ajenda kuelekea mantiki ya kujenga au kuimarisha mfumo wa EUWAWA kwanza. Ujenzi wa mfumo ni lazima ujikite katika kuwezesha serikali, asasi za kiraia na vyuo vikuu kushirikiana na kutoa huduma bora zaidi kwa matokeo mazuri ya ujifunzaji kwa wote, kwa hiyo hufanya kazi kwa kuzingatia viwango. Mifumo ya EUWAWA ni anuwai na tata, na mifumo yote ni tofauti. Kubadilisha mfumo huenda si lazima kubadili matokeo, bali kuuimarisha na kuujenga, na kuufanya ufanye kazi vizuri, ni hatua muhimu katika kutoa matokeo mazuri. Mifumo ina sifa za utendaji na kufanya kazi kwa ufanisi kunahitaji taratibu za kuwezesha vijenzi kufanya kazi pamoja.

Mara nyingi kushindwa kuunganisha vijenzi mbalimbali, au masilahi tofauti miongoni mwa wadau, ndiko husababisha kupungua kwa utendaji wa mfumo, (DEVCO B4 Education Discussion Paper, 2024). Ili kuboresha mfumo, upitiaji matokeo ya mfumo yaliyofanyiwa majaribio kwa kiwango kidogo katika wa Awamu ya Nne (Utekelezaji na Majaribio) ni hatua ya kwanza muhimu. Upitiaji wa mfumo huunda kiungo kikubwa kati ya mwisho wa Awamu ya

Nne na mwanzo wa Awamu ya Tano. Kwa hiyo, upitiaji wa mfumo uliofanyiwa majaribio unatumia michakato na zana kutoka Awamu ya Pili, na tena hufanya tathmini ya jumla ya mfumo mzima kwa pande zote upande wa mahitaji na wa utoaji huduma, ikiwamo kutathmini makubaliano miongoni mwa wabia.

Matokeo ya upitiaji yanahitaji kuchambuliwa, na marekebisho lazima yafanyike ili kuimarisha mfumo na kuufanya ufanye kazi vizuri. Upitiaji unafanywa kwa kuzingatia dira ya mfumo, yaani, nini matokeo yanayotegemewa hapo baadaye? Dira ya mfumo wa EUWAWA iliundwa katika Awamu ya Kwanza na kupitiwa katika Awamu ya Pili ili iingizwe mkabala mpya wa mwitikio wa mfumo wa EUWAWA. Matokeo na mapendekezo ya upitiaji yatatoa mwelekeo kuhusu kanuni ambazo kwazo, mfumo utalazimika kufanya kazi, na seti ya hatua za kuchukua au marekebisho ambayo yataanza kubadilisha mfumo uliopo (uliofanyiwa majaribio katika Awamu ya Nne) kuelekea katika mfumo wa baadaye ambao unaweza kutoa huduma za EUWAWA kwa kiwango kikubwa zaidi na zenye ubora. Kubadilisha mifumo ni kugumu kwa sababu haiwezi kuachwa kabisa, kuundwa upya na kuanzishwa tena. Huduma za EUWAWA ni lazima ziendee kupatikana kwa wakati wote. Mikabala ya kimumo inaweza kusaidia katika mpito huu kwa kuruhusu vitendo vipya kuimarika wakati michakato muhimu ikiendelea. (OECD



Public Governance and Territorial Development Directorate, 2017). Kwa hiyo, jinsi gani ya kufanya marekebisho kwa mfumo uliofanyiwa majaribio kwa mtazamo wa kuupanua mfumo ni sehemu ya pili ya Awamu ya Tano. Kifungu kinachohusu marekebisho kinakopa kutoka kwenye michakato na zana katika Awamu ya Tatu, ambayo inaweza kutumika kutafuta sehemu za kuingilia kwa ajili ya kuuboresha na kuunda upya mfumo wa EUWAWA kwa ajili ya kuupanua.

Kuelewa changamoto na marekebisho yanayohitajika katika mfumo haitoshi. Mara nyingi hatuungalii kinachoweza kufanya kazi kwa kiwango fulani. Je, tunahitaji kuunda upya utaratibu wa kutoa huduma? Au je, ni utendaji wa mfumo kwa upande wa utoaji huduma na ambao utazuia ufanyaji kazi wa mfumo kwa kiwango kikubwa? Hatimaye, tunahitaji kuwa na mfumo wa kitaifa wa EUWAWA ambao unaweza kutoa huduma kwa wanafunzi wa EUWAWA na makundi yaliyolengwa. Tunahitaji kwenda mbali zaidi ya mradi mmojammoja pekee. Mara nyingi tunatoa mifano ya miradi bora ambayo ina mafanikio, lakini muundo wa miradi hii hauangalii masuala ya ubora, ufanisi na uendelevu wa miradi ambao unahitajika kuzidisha miradi hii kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, maana ya kivitendo ya kutafuta mkabala wa upanuzi wa kimfumo ndiyo lengo hasa la sehemu ya tatu ya Awamu ya Tano.

Mpito kutoka Awamu ya Tatu kwenda Awamu ya Nne unategemea sana kukamilika kwa hatua za usanifu na mipango na kuanza kuchukua hatua kwa kutekeleza na kufanya majaribio ya kiwango kidogo cha mfumo mpya uliobuniwa upya. Baadhi ya nchi zinaweza kuwa zimekamilisha muundo wa mwitiko katika mfumo wa EUWAWA pamoja na mpango wa uendeshaji ili kutekeleza mfumo mpya katika Awamu ya Tatu, ilhali wengine wakiwa wamekamilisha tu muundo wa mwitiko katika mfumo. Kwa hiyo, ni vizuri kuwa na ukumbusho mfupi wa maudhui ya muundo wa mwitiko katika mfumo na kufafanua mchakato wa kuandaa mpango wa uendeshaji.


Mpango huu utaandaliwa na kutekelezwa na wadau wa MKMEUWAWA ambao wamekuwa kwenye ubia tangu Awamu ya Kwanza. Kwa kuzingatia mamlaka na umahiri wao, kila mbia atakuwa na wajibu na majukumu tofauti katika mpango. Jambo la muhimu ni masilahi na azima yao ya kushiriki, na sehemu hii ya kijitabu itagusia aina mbalimbali za ushiriki kabla ya kufungua namna utekelezaji utakavyofanyika kutoka upande wa watoa huduma katika sehemu inayofuata.



2. TAFAKURI KUHUSU SAFARI YA MKMEUWAWA: UJUMBE MUHIMU NA DHAMIRA ZINAZOJIRUDIA


Ujenzi wa mfumo wa elimu na ujifunzaji kwa watu wazima (EUWAWA) unachukua muda na ni mchakato endelevu. MKMEUWAWA unazingatia suala hili na unatekelezwa katika awamu tano ambazo zinaweza kuchukua mpaka miaka 12 au zaidi kukamilika, kutegemeana na hadhi ya mfumo wa EUWAWA katika nchi wakati safari ya MKMEUWAWA ilipoanza.

Kwa hiyo, Awamu ya Tano ni kilele cha kazi iliyofanyika katika awamu nne. Angalizo dogo la ujumbe muhimu na dhamira zinazojirudia katika vijitabu vitano vilivyopita na awamu nne vinasaidia katika lengo la kuhakikisha kuwa Awamu ya Tano inajengeka juu ya awamu zilizopita na kwamba dhana muhimu na kanuni za MKMEUWAWA zinazingatiwa.




Kijitabu cha Kwanza: Utangulizi wa Mkabala na Seti ya Zana

- EUWAWA ni sehemu ya duru ya ujifunzaji endelevu na ni sekta mtambuko. Nchi lazima ziingalie mawanda ya EUWAWA ili matumizi ya MKMEUWAWA yazingatie mahitaji yao, changamoto na muktadha.
- Madhumuni ya malengo ya jumla ya MKMEUWAWA ni kuhakikisha kwamba mfumo endelevu wa EUWAWA unakuwapo ambao unaweza kutoa aina mbalimbali za huduma za EUWAWA kwa vijana na watu wazima.
- MKMEUWAWA inategemea seti ya kanuni anuai kama vile kuendeleza mkabala unaojali haki wa EUWAWA, uchangamanishaji wa sekta na masuala na maeneo ya utawala, ushawishi wenye ushahidi, ushirikishaji na ubia, umiliki, kujenga uwezo, na uendelevu.
- MKMEUWAWA unashughulikia vyote, yaani upande wa mahitaji na wa utoaji wa huduma. Lengo la kuboresha utoaji huduma za EUWAWA limeweka mkazo wa mkabala upande wa utoaji huduma wa mfumo. Kwa hiyo, watumiaji wakuu wa mkabala ni kama vile serikali (katika ngazi zote na katika sekta mbalimbali), watendaji wa asasi za kiraia, taasisi za kitaaluma na asasi za kimataifa.
- Katika moyo wa MKMEUWAWA kuna kiunzi cha dhana ambacho kinajumuisha vipengele vinne na vijenzi ishirini vya mfumo madhubuti wa MKMEUWAWA. Kiunzi cha dhana hiki kinavuvia shughuli na michakato yote katika awamu zote za tano za mkabala huu.



Awamu ya Kwanza - Kujenga Makubaliano

- Serikali peke yake haziwezi kukidhi mahitaji ya huduma na zinahitaji kushirikiana na sekta zingine kama vile asasi za kiraia (AZISE, AZAJA, n.k.), vyo viko na sekta binafsi. Asili mtambuko na changamani ya EUWAWA inahitaji mikabala inayogusa sekta nzima.
- Mchakato wa kujenga makubaliano unahitajika kwa wadau wote ili kuwa na dira yenye uelekeo mmoja kuhusiana na nini MKMEUWAWA utafanikisha.
- Kujenga makubaliano ni awamu ya kwanza ya MKMEUWAWA, lakini pia mchakato endelevu ambao unafanyika katika awamu zote za MKMEUWAWA.
- Kujenga makubaliano kunapitia katika hatua kuu tatu:
 - Kipindi cha maandalizi ili kuwashawishi wadau wajihusishe na MKMEUWAWA na ujenzi wa mfumo wa EUWAWA.
 - Mwanzo wa kujenga makubaliano mahususi ya shughuli kama vile kutengeneza dira, n.k.
 - Kuendeleza ujenzi wa makubaliano katika awamu zote za MKMEUWAWA na kufanya kazi kama timu, ubia, n.k.




Awamu ya Pili - Tathmini na Utambuzi

- Mara tu wadau wanapokuwa wamefikia makubaliano kuanzisha ujenzi wa mfumo wa EUWAWA, hali ya mfumo uliopo wa EUWAWA lazima ifanyiwe tathmini. Tathmini inatoa msingi wa taarifa ambazo

zitasaidia katika kuunda mfumo mpya ulioboreshwa.

- Tathmini ya mfumo inafanywa kutoka upande wa mahitaji na upande wa utoaji huduma kwa kuzingatia mkabala wa MKMEUWAWA. Tathmini ya upande wa utoaji huduma inatoa taarifa za kitakwimu na za kitaamuli kuhusiana na hali ya mfumo.
- Mara tu tathmini inapokamilika, uchunguzi lazima ufanyike kuangalia vyanzo vikuu vya vizuizi na kushindwa kufanya kazi kwa mfumo.
- Fikira za kimfumo zinaelekeza mchakato wa uchunguzi na zinasaidia kuelewa mienendo msingi ya mfumo.
- Zana za tathmini na uchunguzi katika Awamu ya Pili zinaweza kutumika muda wowote wakati wa awamu zingine za MKMEUWAWA na kuwa sehemu ya zana za U&T za MKMEUWAWA.




Awamu ya Tatu – Uchambuzi wa Mibadala na Usanifu

- Awamu ya Tatu ni matokeo ya Awamu ya Pili katika mchakato wa ufanyaji wa maamuzi ili kuunda mfumo mzuri na ulioboreshwa. Kila maamuzi yatakayochukuliwa kuna mibadala ya kuzingatiwa na

kulinganishwa na mingine.

- Awamu ya Tatu inajumuisha hatua kuu nne:
 - Tafuta na uweke kipaumbele kwa sehemu bora za kuingilia ili kuboresha mfumo wa EUWAWA.
 - Zingatia mibadala kwa ajili ya kusanifu upya vijenzi vya mfumo vilivyopewa kipaumbele.
 - Tathmini matokeo ya muundo mpya kwa mfumo mzima.
 - Unganisha muundo mpya kwa kufuata mkabala thabiti wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA.
- Zingatia upya majukumu na wajibu, ubia na miundo ya kiutawala ya MKMEUWAWA kama inavyoelekezwa na muundo mpya wa mfumo.





Awamu ya Nne: Utekelezaji na Majaribio

- Awamu ya Nne inatoa fursa ya kutekeleza na kufanyia majaribio mfumo uliosanifiwa upya katika maeneo yaliyochaguliwa na kwa kundi lengwa maalumu kabla ya kupitia, kurekebisha na kupanua katika Awamu ya Tano.
- Mkabala wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA umetafsiriwa katika mpango wa uendeshaji ili kutekeleza na kufanya majaribio ya mfumo mpya.
- Kamati ya kitaifa ya uendeshaji wa MKMEUWAWA imeundwa ili kuongoza utekelezaji na kufanya majaribio ya mfumo mpya. Makundi madogo ya wadau yatafanya kazi katika miradi mbalimbali hasa yale yaliyopangwa kwa mujibu wa vipengele vinne vya mfumo.
- Ushiriki wa wadau katika Awamu ya Nne nzima ni muhimu katika mafanikio ya mfumo mpya.
- Uwezo wa kitaasisi wa kila mdau mmojammoja unaweza kuhitaji kuimarishwa ili kutimiza majukumu na wajibu wao.
- Utekelezaji wa mfumo mpya lazima ufuatiliwe na kutathminiwa kwa uangalifu. Takwimu lazima zirekodiwe katika mfumo wa MUT ili kuitaaruifu Awamu ya Tano.
- Maarifa ya kujifunza na namna bora ya ufanyikaji lazima virekodiwe ili kutoa mwongozo kwa ajili ya uwezekano wa upanuzi.
- Taarifa lazima zikusanywe kutoka upande wa mahitaji ili kujua kama mfumo mpya umeyashughulikia matakwa na masilahi ya kundi lengwa.

Dhamira zinazojirudia katika MKMEUWAWA

- Ujenzi wa mfumo: Mfumo unafahamika kuwa kama chombo chenye vipengele, miundo, michakato mbalimbali ambayo inaungana kwa kupitia njia za mrejesho. Mfumo wa EUWAWA unarejelea mchakato wa kujenga makubaliano miongoni mwa wadau wote muhimu na kutathmini hali ya mfumo, kuchunguza sababu kuu za vizuizi vya mfumo kabla ya kusanifu mfumo mpya ulioboreshwa ambao unawezwa kutekelezwa na kufanyiwa majaribio kwa ajili ya upanuzi kwa kundi lengwa kubwa zaidi na eneo kubwa zaidi la kijiografia.
- Fikra za kimfumo: Fikra za kimfumo ni mkabala wa kimuundo ambao unasisitiza kuchunguza tatizo kikamilifu kabla ya kuandaa na kutekeleza masuluhisho. Fikra za kimfumo ni muhimu katika awamu, hatua na zana zote za MKMEUWAWA.
- Utoaji wa huduma: Utumishi wa umma unaweza kufahamika kama miingiliano yote kati ya serikali na raia iwe huduma zinatolewa moja kwa moja au kupitia vyombo vya kati kama vile asasi za kiraia, sekta binafsi, n.k. Njia mbalimbali za kutoa huduma zipo, lakini lazima ikumbukwe kwamba serikali ndiyo inabaki kuwa na jukumu kubwa. Upande wa utoaji huduma unarejelea wenye jukumu au asasi zinazowajibika kutoa huduma kwa umma. Upande wa wahitaji huduma unarejelea wahasika/wenye wajibu wa kutoa haki kama vile watu binafsi na makundi ambayo yana haki ya kupata na wanaohitaji huduma ya EUWAWA.

3. MUHTASARI WA AWAMU YA UPITIAJI, MAREKEBISHO NA UPANUZI

Awamu ya Tano ya MKMEUWAWA inatekelezwa kwa kupitia hatua na awamu ndogo kuu tatu. Hatua hizo ni:

Upitiaji:

Upitiaji jumuishi lazima ufanyike mwishoni mwa Awamu ya NNE/ na mwanzoni mwa Awamu ya Tano ili kuona kama mfumo mpya uliofanyiwa majaribio unafanya kazi vizuri na kuboresha taarifa kwa kwa kuzingatia hali ya mfumo ya sasa. Hii itawataarifu wadau wa MKMEUWAWA kama mfumo mpya unatoa huduma za EUWAWA ambazo zinakidhi mahitaji ya walengwa wa EUWAWA. Pia, upitiaji huo utatoa maelezo kuhusiana na ushirika wa wadau na uendeshaji wa ubia katika Awamu ya Nne.

Marekebisho:

Upitiaji wa mfumo utatoa maelezo kuhusiana na mapengo, changamoto zilizosalia, utendaji bora na maeneo ya kujifunza na kueleza aina ya marekebisho ambayo yanahitajika kabla ya saula la upanuzi kuzingatiwa. Marekebisho haya lazima yapangwe kwa ajili ya utekelezaji kabla na wakati wa mchakato wa upanuzi wa Awamu ya Tano.

Upanuzi:

Mara tu baada ya wadau wa MKMEUWAWA kujiridhisha kwamba hatua ya mwisho ya mfumo inaweza kutumika katika kiwango kikubwa kwa kuzingatia kundi lengwa na maeneo ya kijiografia, mchakato wa upanuzi (up-scaling) unaweza kuanza.

Kila awamu ya MKMEUWAWA itatoa matokeo mahususi kuhusiana na safari ya ujenzi wa mfumo wa EUWAWA. Matokeo yote haya yatapitwa mwanzoni mwa Awamu ya Tano ili maboresho yaweze kufanywa kwa ajili ya upanuzi (up-scaling). Jedwali la hapa chini linatoa ufafanuzi wa jumla kuhusiana na michakato mikuu mitatu ya Awamu ya Tano:



Awamu	Nini kinatakiwa kupitiwa katika awamu zote nne zilizokamilika za MKMEUWAWA?	Nini kinatakiwa kirekebishwe?	Nini kinatakiwa kupanuliwa?
Awamu ya Kwanza	• Umuhimu na mshikamano wa mawanda na muktadha vilivyofasiliwa vya mfumo wa MKMEUWAWA. • Umuhimu na mshikamano wa dira ya EUWAWA katika awamu zote za MKMEUWAWA. • Miundo ya ubia na utawala wa MKMEUWAWA na majukumu na wajibu wa wadau. • Uhusiano wa wadau na kiwango cha makubaliano kuhusu mfumo wa EUWAWA/mchakato wa MKMEUWAWA. • Usimamizi wa ujenzi wa makubaliano kupitia kufanya kazi kama timu, usimamizi wa migogoro na upatanisho. • Maendeleo ya jumla kuhusu mchakato wa ujenzi wa mfumo wa EUWAWA kwa mujibu wa mpango wa MKMEUWAWA kuanzia Awamu ya Kwanza mpaka Awamu ya Nne.	Kwa kuzingatia matokeo ya upitiaji katika awamu zote marekebisho yafuatayo yanaweza kutakiwa kufanywa kabla upanuzi haujafanyika. Zingatia kwamba marekebisho hayajaorodheshwa kwa kuzingatia awamu, kwa kuwa yanaathiri mfumo kwa jumla, ila jaribio limefanyika ili kuonesha ni awamu ipi yanatokea. • Mawanda na muktadha wa mfumo wa EUWAWA. Je, baadhi ya makundi lengwa au huduma zinahitaji kujumuishwa? • Je, dira ya EUWAWA inatakiwa kusasishwa? • Miundo ya utawala ya MKMEUWAWA/ubia mbalimbali katika sekta na maeneo ya utawala. • Kiwango cha makubaliano. • Vijenzi vya mfumo ambavyo vimetekelezwa katika Awamu ya Nne lakini bado havifanyiwakazi vizuri ndani ya mfumo. • Vijenzi bora ambavyo vinatakiwa kuwekwa. • Aina ya huduma ambazo mfumo wa EUWAWA huwa unazitoa na/ au taratibu za utoaji huduma za EUWAWA. • Muundo wa mfumo wa EUWAWA uliotekelezwa katika Awamu ya Nne wa weza kuhitaji kusasishwa na marekebisho kabla ya kuandikwa kama muundo wa mwisho wa mfumo na upanuzi uweze kufanyika. • Kanuni za msingi ambazo zinaelekeza mfumo wa EUWAWA. • Uanzishwaji wa viwango na vigezo unaweza kufikiriwa kuzingatiwa. • Kujenga uwezo wa kitaasisi na kibinafsi. • Mfumo wa U&T kwa ajili ya mfumo wa EUWAWA, ukijumuisha MUT. • Taratibu za kushirikisha na maarifa, namna bora na kuyajumuisha kwa msingi endelevu.	Hatimaye muundo mpya wa mfumo wa EUWAWA unapaswa kukubaliwa kwa ajili ya upanuzi. Masuala tofauti ya naathiri upanuzi. Hatua kadhaa zinapaswa kufuatwa na mazingatio yanazingatiwa ili kuwezesha mchakato huo. Kwa kuzingatia upitiaji wa mfumo na marekebisho yanayotakiwa, yafuatayo ni baadhi ya masuala muhimu yatakayozingatiwa wakati wa kupanua mfumo: • Kwa kuzingatia dira ya mfumo wa EUWAWA kama nyenzo ya kuongoza upanuzi. • Kupanua kundi lengwa la EUWAWA kwa vigezo vya aina na idadi. • Kupanua kundi lengwa la EUWAWA kwa vigezo vya mahali na maeneo ya kijiografia. • Kushirikisha sekta na wabia zaidi ili kutoa huduma za EUWAWA. • Vigezo vya vijenzi vya mfumo wa EUWAWA, kwa mfano, upangaji na bajeti vitafanyikaje ndani ya mfumo wa kitaifa, n.k.? • Mazingatio ya kujenga uwezo na kuzifanya asasi na watu binafsi kuwa na utaalamu ndani ya mfumo wa EUWAWA. • Mifumo ya U&T na MUT na kuzingatia uanzishwaji wa mifumo ya kidijiti, n.k. Sehemu ya sita katika kijitabu hiki inaeleza kwa kinamchakato wa upanuzi wa mfumo wa EUWAWA katika ngazi ya kitaifa.
Awamu ya Pili	• Hali ya mfumo wa EUWAWA upande wa utoaji huduma: Je, vijenzi vipo, ni namna gani mfumo unafanya kazi vizuri? • Mitazamo kutoka kundi lengwa la EUWAWA (upande wa wahitaji huduma) kuhusu aina za huduma, ubora, ufikikaji, n.k. • Je, sababu kuu na vizuizi vimeshughulikiwa? (Kama ilivyoelezwa katika taarifa ya uchunguzi).		
Awamu ya Tatu	• Ufanisi wa muundo wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA na muundo wa mfumo mpya katika kushughulikia changamoto za mfumo uliopita? • Je, kanuni za msingi zilizokubaliwa za mfumo zimefuatwa, kwa mfano, umiliki, n.k.?		
Awamu ya Nne	• Je, mpango wa utendaji katika Awamu ya Nne unatafsiri muundo wa mfumo mpya wa EUWAWA katika mpango wa utekelezaji wa mradi na programu ya kivitendo na inayowezezekana? • Ufanisi wa ushirikiano wa wadau ndani ya muundo wa utawala na ubia ulirasimishwa? • Je, wadau / wabiawa MKMEUWAWA walijengewa uwezo wa muhimu kitaasisi na kibinafsi ili kutekeleza mpango wa utendaji na mfumo mpya wa EUWAWA? • Ni kwa kiwango gani mfumo wa U&T unaonesha maendeleo na changamoto katika utekelezaji wa mpango wa utendaji na ufanyaji kazi wa mfumo mpya kutoka upande wa mahitaji na utoaji huduma? • Je, MUT umekuwa unafikiwa na wabia wote wa MKMEUWAWA na taarifa zimetumikaje? • Je, wadau wa MKMEUWAWA wamepata fursa za kufanya tafakuri na kujumuisha maarifa ya kujifunza na namna bora wakati wamajaribio na utekelezaji wa mfumo mpya katika Awamu ya Nne? Kwa vipi? • Je, tafiti zozote za tathmini kama vile upimaji mbalimbali wa hali ya mfumo, uchunguzi au changanuzi kifani zimefanyika katika Awamu ya Nne? Je, matokeo yake yametumikaje?		

Zingatia:

Jedwali linajaribu kuonesha maudhui ya michakato katika kila moja ya hatua ndogo tatu za awamu ya tano, lakini hakuna vipimo tofauti kabisa ambavyo vitaonesha waziwazi ni wapi hatua moja inaishia na inayofuata inanzia. Mbali na kuwa na ripoti za mwisho za upitiaji, hatua za marekebisho na upanuzi zinaweza kwenda pamoja na kukiwepo na uwezekano wa baadhi ya shughuli za hatua hizi mbili kuingiliana. Zaidi ya hayo, kama itakavyo fafanuliwa baadae katika kijitabu, upanuzi unaweza kuwa tayari umeanza wakati wa majaribio katika awamu ya nne.

4. KUPITIA MATOKEO YA AWAMU YA KWANZA HADI AWAMU YANNE

4.1 Utangulizi wa mchakato wa upitiaji.

Dhana ya “Upitiaji” inatumika kuelezea aina yoyote ya tathmini au utafiti utakaofanywa kama shughuli ya ndani na wabia wa MKMEUWAWA wenyewe au na wakaguzi wa nje au wote, Katika muktadha wa MKMEUWAWA ukiangalia umiliki wa michakato na maamuzi, inapendekezwa kwamba muunganiko wa tathmini zote mbili. Yaani ile ya ndani na ya nje zitumike. Fasili ya “Upitiaji” kama ilivyoelezwa katika Oxford Advanced Learners’s Dictionary (Jonathan Crowther, 1999) kiwango cha upitiaji katika awamu ya tano ijulikanayo kama “Kuchunguza au kuzingatia kitu kwa uwezekano wa kukibadilisha kama kitaonekana kinafaa au cha umuhimu”, kimefafanuliwa vizuri. Hii ni muhimu ikizingatiwa kwamba ifanyike kwenye mfumo wa EUWAWA kwa lengo la kuelewa marekebisho katika maandalizi ya upanuzi. Hivyo basi, neno “upitiaji” na “tathmini” yatumika kwa pamoja kwa kupokezana yakimaanisha kitu katika hatua ya tano.

Mapitio mwishoni mwa awamu ya nne/ na mwanzoni mwa awamu ya tano yatachukua sura ya tathmini kwamba yanapima umuhimu, ubora, ushikamani, ufanisi, athari/matokeo na uendelevu wenye tija wa mfumo wa EUWAWA uliofanyiwa majaribio (Awamu ya nne). Yatajikita zaidi katika mafanikio ya malengo yaliyokusudiwa vilevile kuangalia uwezekano wa kufikia dira ya mfumo wa EUWAWA iliyopitia michakato yote iliyokuwepo katika awamu ya kwanza, ya pili na tatu. Mfumo uliofanyiwa majaribio katika awamu ya nne umekuwa ndiyo kiini kikubwa cha upitiaji/tathmini.




Kiunzi dhana cha MKMEUWAWA chenye vipengele vinne vya mfumo na vijenzi ishirini pamoja na misingi, dhana na muktadha ambao unafafanua mkabala unabaki kuwa mkabala wa rejea kwa ajili ya upitiaji/tathmini.

Tathmini mbalimbai za shughuli au matukio zimebainishwa katika kijitabu cha awamu ya nne ya MKMEUWAWA kama ilivyoelezwa hapa chini (rejea kipengele namba 3.4 katika kijitabu cha nne (Utekelezaji na majaribio).

- Tathmini zinazoendelea kama upitiaji wa kipindi fulani kwa taasisi na wabia wakati wa utekelezaji hukusanya taarifa kwa njia zisizo rasmi zaidi, kwa mfano, wakati wa mkutano wa tafakuri ya washirika kuhusiana na utekelezaji wa mfumo uliofanyiwa majaribio, kwa kutumia taarifa za mfumo wa MUT na ripoti kutoka duru za tafiti zisizo za kitakwimu.
- Tafiti za msingi kama vile tathmini ya mfumo wa EUWAWA ambayo ilifanyika kwa kupitia upitiaji taalimu kwa matokeo ya kitakwimu na ya kitaamuli matakwa ya walengwa wa EUWAWA kuhusiana na mahitaji ya tathmini. Wakati wa awamu ya pili ya MKMEUWAWA.
- Upitiaji wa nusu muhula kwa kawaida hufanyika katikati kupitia miradi /programu na kujikita zaidi katika utendaji hata kama mradi/programu inayoendelea inaonekana kuelekea kufikia au kutofikia malengo. Washirika wa MKMEUWAWA watakuwa wamefanya tathmini ya nusu muhula wakati wa awamu ya nne ya hatua ya utekelezaji, hususani ni kama awamu ya majaribio ya mfumo mpya itakuwa imechukua muda mrefu zaidi ya miaka mitatu.
- Tathmini tamati ni tathmini ya ndani au ya nje kuonesha kama mradi/programu imefikia malengo na kutoa matokeo ya haraka ambayo yanaweza kuangaliwa baina ya kundi lengo.
- Tathmini tangulizi au tathmini ya baadaye mara nyingi hufanyika baada ya programu kuhitimishwa na kujikita katika athari za muda mrefu kuhusiana na maisha ya wanufaika na mazingira, n.k.

Upitiaji mwishoni mwa awamu ya nne/mwanzoni mwa awamu ya tano unaweza kuelezewa vizuri kama muunganiko wa upitiaji wa nusu muhula na upitiaji tamati/wa mwisho wakati pia unaingiza vipengele vya aina nyingine za tathmini. Sababu ni kama ifuatavyo:

- Mchakato wa ujenzi wa mfumo wa EUWAWA kwa kutumia MKMEUWAWA bado haujafanyika na hali ya utendaji kazi wa mfumo wa majaribio kutoa awamu ya nne bado iko chini ya upitiaji kwa ajili ya maboresho/mabadiliko kabla ya upanuzi. Katika muktadha huu, tathmini inachukua kutoka kwenye misingi ya mfumo na nyenzo za tathmini ya nusu muhula.
- Mradi wa majaribio umetekelezwa kwa muda mrefu wa kutosha kiasi cha kutoa mahitimisho iwapo umefikia malengo yake, uwezeakano wa kufanikisha dira ya EUWAWA na baadhi ya athari za hapohapo kwa walengwa. Kutegemeana na hali ya mfumo katika nchi mbalimbali na muundo mpya wa mfumo unaotakiwa kufanyiwa majaribio, mchakato wa majaribio unaweza kuchukua miaka mitatu hadi sita. Katika suala hili, upitiaji unaazima maswali ya utafiti na mbinu kutoka kwenye muundo wa tathmini ya muhula/ya mwisho.
- Taarifa za msingi zilizokusanywa kutoka upande wa mahitaji na utoaji huduma katika awamu ya pili lazima zitumike kwa lengo la ulinganishaji, kwa mfano, je, alama za mfumo zilibadilika? Je, maelezo kuhusu vijenzi vya mfumo yanaonesha kwamba mfumo unafanya kazi na kutoa huduma?
- Kama ilivyo kwa tathmini yoyote ile upitiaji lazima ubebe taarifa kutoka katika upitiaji na tafiti zozote zilizofanyika kama tathmini zinazoendelea, tafiti za uchanganuzi kifani na uchunguzi ambazo inaziba pengo la Ufuatiliaji na Tathmini, pamoja na taarifa katika Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa (MUT).



Ingawa mfumo uliofanyiwa majaribio katika awamu ya nne umetekelezwa na wabia wa MKMEUWAWA katika mfumo wa vikundi vya miradi iliyopangwa kwa kuzingatia vipengele vinne vya mfumo na kufungwa pamoja chini ya mwamvuli wa mkabala wa usimamizi wa programu ya MKMEUWAWA (Rejea awamu ya nne, sehemu 2.2), shughuli zinazofanyika ndani ya mradi na programu hasa zinazochangia kwenye majaribio ya kina ya mfumo wa EUWAWA kama ilivyoainishwa katika mkabala wa kimwitikio wa mfumo sanifu wa EUWAWA. Kwa hiyo, upitiaji usiangaliwe tu kama mradi/programu halisi iliyofanyiwa tathmini bali lazima ijikite katika kuonesha ni kwa kiwango gani utoaji wa huduma za EUWAWA ni endelevu katika mfumo wa EUWAWA. Kwa hiyo, timu ya upitiaji lazima iazime zana kutoka fani ya utawala wa umma na serikali za mitaa ili kupata utoaji huduma na semina elekezi kuhusu mfumo.

Shughuli zilizofanyika katika awamu ya kwanza hadi ya nne zimetoa matokeo makubwa, matokeo na taarifa kuhusiana na mfumo wa EUWAWA na jinsi unavyofanya kazi. Kumbuka kwamba taarifa hizi zimekusanywa kwa zaidi ya miaka 12 au zaidi, na zinashirikisha wabia mbalimbali, sekta na maeneo mbalimbali ya utawala. Zaidi ya hayo, zimejumuisha utekelezaji wa mfumo katika miradi midogomidogo ndani ya mfumo mpana wa programu. Kufanya upitiaji wa hali na ufanisi wa mfumo mwishoni mwa Awamu ya Nne na mwanzoni mwa Awamu ya Tano, siyo kitu rahisi. Inaweza kuchukua miezi miwili au mitatu zaidi, kama siyo zaidi, kukamilisha kwa kuwa utalenga masuala mbalimbali ya mfumo, kama itakavyooneshwa katika sehemu inayofuata.

Mchakato mzima wa upitiaji hauwezi kufunguliwa ndani ya mawanda ya kijitabu hiki, lakini majaribio yanafanywa ili kutoa mwongozo ambao utapendekeza zana na vifaa, vinong'onezo na vidokezo ambavyo vitasaidia wabia wa MKMEUWAWA kwenye nchi mbalimbali katika kutekeleza mchakato. Mahali pazuri pa kuanzia ni kuuliza maswali ya msingi ya "kwa nini, lini, wapi, nini, nani, na vipi". Sehemu inayofuata inalenga kuwapatia watumiaji wa MKMEUWAWA mwongozo wa namna ya kuandaa usanifu wa mchakato wa upitiaji.

4.2. Kusanifu mchakato wa upitiaji

Mada zifuatazo zitapitiwa ili kushughulikia usanifu wa mchakato wa upitiaji:

- Hatua katika kusanifu na kutekeleza upitiaji.
- Kujibu maswali ya msingi kuhusu upitiaji kama vile ni nini upitiaji unapaswa kushughulikia, nani atafanya upitiaji, kwa jinsi gani, na lini, n.k?
- Kuchanganua jinsi gani ya kufanya kutoka upande wa mahitaji na upande wa utoaji huduma na kufanya upitiaji wa ubia na mchakato wa MKMEUWAWA.

4.2.1 Hatua katika kusanifu na kutekeleza upitiaji

Upitiaji utajumuisha hatua/awamu zifuatazo (EuropeanAid Co-operation Office Joint Evaluation Unit, 2006):

- Awamu ya maandalizi ambapo wakati huo wabia wa MKMEUWAWA wataandika hadidu za rejea, waajiri timu ya nje ya upitiaji na/au kuchagua timu ya ndani ya upitiaji. Mbinu za kina za upitiaji na maswali vitaandaliwa katika awamu hii.
- Awamu ya kazi ya mezani ambapo wakati huu timu ya upitiaji (ya ndani na ya nje) itapitia nyaraka zote za mchakato wa MKMEUWAWA zilizozalishwa tangu awamu ya kwanza na hususani ni kipindi cha awamu ya nne. Nyaraka hizi zitajumuisha yafuatayo:
 - Makubaliano ya ubia na mkataba wa maelewano.
 - Mpango wa uendeshaji wa MKMEUWAWA ulioandaliwa katika awamu ya kwanza, ambao unaonesha jinsi awamu zote zitakavyotekelezwa na hatua muhimu mbalimbali kwa kipindi fulani.
 - Ripoti mbalimbali kutoka kwenye warsha kadhaa na mikutano kuanzia awamu ya kwanza hadi ya nne.
 - Tathmini ya mahitaji iliyofanyika katika awamu ya pili kama taarifa za msingi.
 - Tathmini ya upande wa mahitaji ya huduma iliyofanywa pamoja na upitiaji taarifa katika awamu ya pili (taarifa za kitakwimu na za kitaamuli) kuhusiana na hali ya mfumo) kama taarifa za msingi.
 - Ripoti ya warsha ya uchunguzi katika awamu ya pili inayoonesha visababishi vikuu na changamoto kubwa ambazo mfumo mpya unapaswa kuzishughulikia.
 - Mkabala wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA kutoka awamu ya tatu, vikiwemo maelezo ya dira na malengo ya mfumo mpya wa EUWAWA, muundo wa utawala, n.k
- Mpango wa uendeshaji kutoka awamu ya nne ukijumuisha mipango ya mradi mmojammoja wa makundi ya wabia wanaofanyia kazi vipengele mbalimbali vya mfumo na mfumo wa usimamizi wa programu ya MKMEUWAWA.
- Taarifa kutoka mfumo wa U&T wakati wa majaribio, ripoti za wabia, taarifa za mikutano, ripoti za duru bora za kujifunza, na upitiaji au tathmini zozote zilizofanyika katika awamu ya majaribio, n.k.
- Awamu ya uwandani ambapo timu za upitiaji zitafanya mahojiano na kundi lengwa la EUWAWA, wabia watekelezaji, wadau wakuu na kuhakikisha kwamba taarifa msingi zinakusanywa, zinachambuliwa na kujibu malengo ya upitiaji.
- Awamu ya majumuisho na uchambuzi ambapo timu ya upitiaji itachambua taarifa (data msingi na data za upili) na kuandaa ripoti ambayo inajumuisha matokeo na hitimisho kuhusiana na maswali yaliyoulizwa pamoja na tathmini nzima. Hii pia itajumuisha mapendekezo ambayo yatawasaidia wadau wa MKMEUWAWA katika hatua ya marekebisho katika awamu ya tano. Mara tu wadau wa MKMEUWAWA watakaposoma ripoti na kutoa mrejesho kwa timu ya wapi-tiaji, masahihisho/marekebisho ya lazima yanaweza kufanyika na ripoti itahitimishwa. Zingatia kwamba upitiaji wa ripoti unaweza kufanyika katika sehemu au vipengele mbalimbali kulingana na mawanda ya mfumo wa EUWAWA, kwa mfano, upitiaji wa upande wa mahitaji na utoaji wa huduma kila mmoja pamoja na upitiaji kuhusu ubia. Hii inamaanisha kwamba mara tu baada ya kila ripoti ya upitiaji kuwa imekamilishwa kama ilivyoelezwa hapo juu, timu kuu ya watathmini (wa ndani/nje) bado itapaswa kuandaa ripoti kubwa kuhusu mfumo wa EUWAWA. Sehemu ya 4.3 inatoa mfumo wa kuisaidia timu katika jukumu hili.
- Awamu ya usambazaji na ufuatiliaji ambapo ripoti mbalimbali ambazo zina muhtasari wa jumla zitawasilishwa kwa wabia wote wa MKMEUWAWA, hususani kwa viongozi waandamizi, katika warsha au mfululizo wa matukio ya uchambuzi na kufanya uamuzi katika hatua ya marekebisho ya Awamu ya Tano. Sehemu ya tano ya kijitabu hiki inaelezea jinsi gani matokeo ya upitiaji/tathmini yatatumika katika kufanya marekebisho ya mfumo wa EUWAWA kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi.

4.2.2 Kujibu maswali muhimu kuhusu upitiaji

Kujibu maswali ya msingi kuhusiana na upitiaji itawapa wabia wa MKMEUWAWA taarifa ambazo zitatumika kuandikia habibu za rejea kwa ajili ya mchakato wa upitiaji na kuanza upitiaji wenyewe.

Kwa nini upitiaji ni muhimu?


Upitiaji unahitajika ili kuona kama mfumo uliofanyiwa majaribio unafanya kazi vizuri kiasi kwamba unaweza kupanuliwa au kama marekebisho/maboresho zaidi yanahitajika. Je, mfumo unafikia malengo yake na uwezekano wa kufanikisha dira ya mfumo wa EUWAWA? Hili ndilo lengo kuu la upitiaji/tathmini.

Je, upitiaji utafanyika lini?

Upitiaji lazima upangwe na kufanyika mwishoni mwa awamu ya nne na unaunda hatua au awamu ndogo ya kwanza ya awamu ya tano ya MKMEUWAWA.

Je, upitiaji utafanyika wapi?

Mfumo uliofanyiwa majaribio katika awamu ya nne ulisanifiwa ili kutatua changamoto muhimu ya makundi lengwa ya EUWAWA ambayo yanawakilisha kundi lengwa la kitaifa pamoja na maeneo mbalimbali ya kijiografia ambayo yanatoa fursa za kimajaribio ili kutathmini uwezekano wa kutekeleza mfumo katika ngazi ya kitaifa. Kwa hiyo, upitiaji lazima uelekezwe kwenye maeneo yaliyofanyiwa utafiti na pia kwa makundi lengwa kwa mujibu wa muundo na mpango wa uendeshaji wa awamu ya nne. Pia, unapaswa kufanyika katika maeneo yote ya utawala, kuanzia ngazi ya taifa mpaka ngazi ya mtaa kuhusiana na muundo wa utawala katika nchi. Watathmini wanaweza kuamua kujumuisha makundi ya udhibiti ambapo majaribio ya mfumo hayajatekelezwa ili kuwa na taarifa linganishi kuhusu namna gani nzuri mfumo unafanya kazi na kutoa huduma ubora.



Nani wanapaswa kufanya upitiaji?

Ama kwa hakika, upitiaji utafanywa na mchanganyiko wa timu ya watathmini wa ndani na wa nje wakati sehemu nyingine zitafanywa na wabia wa MKMEUWAWA na nyingine kwa kupitia washauri elekezi. Ni muhimu kwamba wabia wa MKMEUWAWA wanachukua umiliki wa mchakato wa upitiaji kwa kuandaa hadibu za rejea, kuajiri washauri elekezi na kuunganisha timu ya wawakilishi wa ndani kutoka wadau/wabia wote na kusimamia mchakato kwa ushirikishaji wa kundi rejea, kwa mfano, kamati ya kitaifa ya uendeshaji wa MKMEUWAWA. Hatimaye, matokeo ya upitiaji yanapaswa kuaminiwa na kutumiwa na wabia wa MKMEUWAWA. Kamati ya uendeshaji ya MKMEUWAWA inayojumuisha wabia wote wa MKMEUWAWA inapaswa kushika jukumu kubwa la uendeshaji.

Mawanda ya upitiaji ni makubwa na yanajumuisha upande wa mahitaji na wa utoaji huduma wa mfumo pamoja na miundo ya utawala na uhusiano wa ubia. Kwa hiyo, unaweza kuhitaji timu kadhaa za upitiaji ili kuchukua wajibu katika sehemu mbalimbali za upitiaji. Timu hizi lazima zifanye kazi ndani ya mfumo mpana ili kuhakikisha kwamba majumuisho na uchambuzi wa matokeo na mapendekezo yanatatua changamoto za mfumo mzima wa EUWAWA. Itahitaji viongozi wa timu wenye uzoefu na maarifa. Sehemu inayofuata inalezea kile ambacho kitatakiwa kupitiwa na inatoa mwelekeo wa timu za upitiaji ambazo zinapaswa kutafutwa/kuchaguliwa ili kufanya upitiaji.

Nini kinafanyiwa upitiaji?

Jedwali katika sehemu ya tatu linaonesha nini kinapitiwa katika awamu zote za MKMEUWAWA. Orodha ya matokeo inaweza kupangwa katika makundi yanayofanana ambayo yatashughulikiwa kwa kina zaidi katika sehemu ndogo zilizobakia za mchakato wa upitiaji. Ama kwa hakika, wabia wa MKMEUWAWA wanapaswa kujumuisha na kuingiza vigezo vya tathmini vya OECD (Tazama ukumbusho kuhusu vigezo hivyo katika ukurasa wa 20) katika hadidu za rejea kwa makundi tofauti ya upitiaji katika ukurasa unaofuata. Muhtasari wa matokeo yatakayofanyiwa upitiaji ni:

Upande wa mahitaji na utoaji wa huduma za mfumo wa EUWAWA uliofanyiwa majaribio

- Umuhimu wa jumla, ufanisi na mshikamano wa mfumo mpya wa EUWAWA uliofanyiwa majaribio ili kutatua changamoto ya mfumo uliopita. Je, visababishi vikuu na changamoto vimetatuliwa? Kwa kiwango gani?
- Hali ya mfumo wa EUWAWA kutoka upande wa utoaji huduma: Je, vijenzi vipo, je, ni kwa jinsi gani mfumo unafanya kazi vizuri? Nini mitazamo kuhusiana na uendeleu wa mfumo na utaasisishaji wa mfumo?
- Mtazamo kutoka kwa kundi lengwa la EUWAWA (upande wa mahitaji/watumiaji) kuhusiana na aina za huduma, ubora, ufikiwaji n.k. Je, ni athari gani za moja kwa moja za mfumo uliofanyiwa majaribio katika maisha ya kundi lengwa?
- Je, kanuni za msingi zilizokubalika za mfumo zimefuatwa? Kwa mfano umiliki n.k.?
- Je, mpango wa uendeshaji katika awamu ya nne umetafsiri mfumo mpya wa EUWAWA uliosanifiwa upya katika mpango wa utekelezaji wa kivitendo wa miradi na programu zinazoonekana?
- Ni kwa kiasi gani mfumo wa U&T ulibainisha maendeleo na changamoto katika utekelezaji wa mpango wa uendeshaji na utendaji kazi wa mfumo mpya wa EUWAWA kwa upande wa mahitaji na wa utoaji huduma.
- Je, MUT umeweza kufikiwa na wabia wote wa MKMEUWAWA na je, taarifa zimetumikaje?
- Je, kuna utafiti wowote wa tathmini kama vile tathmini ya hali ya mfumo, tafiti za kiuchunguzi au za uchanganuzi kifani ambazo zimefanywa wakati wa awamu ya nne? Je, matokeo ya utafiti yametumikaje?
- Je, mabadiliko na marekebisho gani yanahitajika?

Wadau na wabia.

- Je, kuna uhusiano gani miongoni mwa wadau na kiwango gani cha makubaliano kuhusiana na mfumo wa EUWAWA/mchakato wa MKMEUWAWA?
- Je, ni ubia wa aina gani wa MKMEUWAWA ulioundwa na upo kiwango gani cha kutaasisishwa?
- Je, wadau/wabia wa MKMEUWAWA walijengewa uwezo katika ngazi ya taasisi na watu binafsi ili kutekeleza mpango wa uendeshaji na mfumo mpya wa EUWAWA?

Mchakato wa MKMEUWAWA

- Je, wadau wa MKMEUWAWA walipata fursa ya kutafakari na kuingiza mambo ya kujifunza na njia bora wakati wa majaribio na utekelezaji wa mfumo mpya katika awamu ya nne?
- Je, ni maendeleo gani ya jumla kuhusiana na mchakato wa kujenga mfumo wa EUWAWA kwa kuzingatia mpango wa MKMEUWAWA kuanzia Awamu ya Kwanza hadi Awamu ya Nne? Je, malengo yamefikiwa? Je, nini mafanikio na changamoto?



Je, upitiaji unapaswa kufanyika kwa njia gani?

Mawanda ya upitiaji ni mapana si tu kwa kigezo cha maudhui ya kile kinachopaswa kupitiwa bali pia kwa idadi ya wabia wanaohusika, kundi lengwa la EUWAWA na maeneo ya kijiografia yatakayohusishwa, kutegemeana na muundo wa majaribio. Katika kuandaa hadidu za rejea kwa ajili ya upitiaji, uamuzi lazima ufanyike kwa kuzingatia:

- Malengo makuu ya upitiaji.
- Mawanda na muundo wa sampuli bila kujumuisha ukusanyaji wa data kuhusiana na mada kuu na dhamira za mfumo wa EUWAWA.
- Jinsi ya kugawanya upitiaji katika sehemu mbalimbali (m.f., upande wa mahitaji na upande wa utoaji huduma na ubia mbalimbali), wakati huohuo kuendelea kuhakikisha kwamba kuna mshikamano na ufungamano katika ripoti kuu ya mwisho.
- Aina ya timu ya upitiaji iliyohitajika (kwa mfano, watathmini wa ndani/wa nje au mjumuiko wa wote).
- Mapendekezo kuhusiana na mbinu. Mfano, upitiaji taalimu, data msingi na data za upili, kutoa kipaumbele kwa mbinu shirikishi, n.k.
- Maswali ya utafiti.
- Muda ulipangwa kwa ajili ya upitiaji.

Timu za upitiaji lazima ikubaliane na kanuni za utafiti kama vile mbinu mseto. Kufanya marudio na uhalali, wakati huohuo wakitambua na kufanya kazi ndani ya mipaka ambayo inaweza kuwepo katika timu. Vijitabu vya Awamu ya Kwanza hadi ya Nne vya MKMEUWAWA vinatoa mifano ya zana na mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika katika kufanya upitiaji. Sehemu ya 4.2.3 itaelezea kuhusu na kurejelea mfumo kutoka upande wa mahitaji na utoaji huduma ikiwemo upitiaji wa ubia wa MKMEUWAWA na muundo wa utawala.

Kumbukumbu kuhusiana na vigezo sita vya tathmini vya OECD (OECD DAC, 2019):**Umuhimu**

Kwa kiasi gani mfumo wa EUWAWA ulioundwa uliitikia kundi lengwa upande wa mahitaji na wabia wa MKMEUWAWA upande wa utoaji huduma na kuendelea kufanya hivyo kama hali ikibadilika? Hii inamaanisha kwamba utekelezaji wa muundo na majaribio ya mfumo mpya wa EUWAWA unaendana na uchumi, mazingira, masuala ya kijamii, siasa na hali ya uwezo ambamo mfumo unajitokeza. Pia, inachunguza kwa kiasi gani malengo ya majaribio ya mfumo na muundo vimezingatia sera na vipaumbele vya nchi. Kwa hiyo, umuhimu unaweza kutathminiwa kwa kuzingatia muktadha wa vipengele na vijenzi vya MKMEUWAWA kwa kuunganisha na upande wa mahitaji na wa utoaji huduma. Inahitaji kufanya uchambuzi wa mabadiliko katika muktadha kutathimini mawanda ambayo mfumo unaweza au umesasishwa ili kubakia muhimu. Umuhimu endelevu wa mawanda na muktadha wa EUWAWA uliofasiliwa kama ilivyokubaliwa na wabia wa EUWAWA unapaswa kuchunguzwa. Tathmini ya upande wa mahitaji itathibitisha hili au kubainisha mabadiliko yanayohitajika.

Mshikamano.

Ni kwa jinsi gani hatua mbalimbali zilizochukuliwa/muundo wa mfumo na majaribio vinafaa katika muktadha mzima wa nchi? Mshikamano unarejelea ushirikiano wa mfumo wa EUWAWA na hatua nyingine zilizochukuliwa nchini, sekta au taasisi. Aidha, unarejelea mshikamano wa ndani na wa nje. Mshikamano wa ndani unashughulikia mfungamano na mwingiliano katika hatua iliyochukuliwa na hatua zingine zilizochukuliwa na taasisi ileile. Kumbuka kwamba wabia wa MKMEUWAWA walifanya kazi katika makundi yao kwa kuzingatia mipaka ya

vipengele vya mfumo wa MKMEUWAWA na kutekeleza miradi mbalimbali katika kufanya majaribio ya mfumo mpya uliosanifiwa. Kijitabu cha awamu ya nne kinasisitiza kwamba majaribio lazima yawekwe kwenye mfumo uliopo kadiri inavyowezekana kwa ajili ya uendeleu wa baadaye. Kigezo cha mshikamano kitachunguza suala hili. Mshikamano wa nje unazingatia uwiano na hatua zilizochukuliwa na watendaji wengine katika muktadha uleule na utajumuisha uoanishaji na uratibu.

Ufanisi.

Kiwango ambacho mfumo uliojaribiwa ulifikia au unatarajiwa katika kutimiza malengo yake, yakiwemo matokeo yoyote yanayoonesha tofauti katika makundi yote. Mkabala wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA unajumuisha dira na malengo kwa ajili ya mfumo kufanyiwa majaribio. Ingawa ni mapema sana kutathmini kama mfumo unaweza kufikia dira yake, ni muhimu angalau kuchunguza iwapo muundo mpya ulichangia kiwango kikubwa cha matokeo ya malengo.

Tija.


Tija inarejelea ni kwa jinsi gani rasilimali zinatumika vizuri. Je, mfumo unatoa au unatarajiwa kutoa matokea kwa muda uliopangwa? Hii inajumuisha kutathmini tija ya kiuendeshaji, kwa maneno mengine jinsi gani utekelezaji wa majaribio ya mfumo umesimamiwa miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA. Tija ni muhimu zaidi kwenye vijenzi chini ya vipengele vya michakato ya usimamizi wa mfumo na utaratibu wa kitaasisi na namna gani vijenzi hivi na vipengele vinaleta matokeo chini ya michakato ya kitaalamu ambapo huduma zinalifikia kundi lengwa. Taarifa kuhusu gharama za kutoa huduma za EUWAWA na namna huduma hizi zinavyoweza kufikishwa kwa namna bora zaidi itasaidia katika michakato ya kupanga na kuweka bajeti wakati wa mchakato wa upanuzi.

Athari.

Hii inarejelea ni kwa kiwango gani mfumo na utoaji wa huduma umetoa au unatarajiwa kutoa athari za hali ya juu ambazo ni chanya au hasi, zinazotarajiwa au zisizotarajiwa. Kwa maneno mengine, 'Ni tofauti gani, au ni maboresho gani ya mfumo yanafanya?' Athari hizo zinashughulikia umuhimu mkubwa na mabadiliko tarajiwa yanayotokana na maboresho hayo. Kwa mfano, je, huduma za EUWAWA zilizotolewa na kupokelewa na kundi lengwa zimeleta mabadiliko katika mkondo wa elimu na fursa za maisha ya watu? Athari zinachunguza mabadiliko ya jumla na ya kudumu katika mifumo na miiko na matokeo muhimu yanayotarajiwa katika maisha ya watu. Ingawa, upitaji hautaweza kutathmini athari kwa undani zaidi. Lazima uchunguze athari za hapohapo kuhusu mfumo na huduma zilizotolewa ili kujua iwapo muundo wa mfumo uko kwenye mwelekeo sahihi au unahitaji marekebisho.

Uendeleu

Uendeleu unachunguza kwa kiasi gani faida za mfumo ulioboreshwa zitaendelea au zinaelekea kuendelea. Unajumuisha uchunguzi wa masuala ya fedha, kiuchumi, kijamii, kimazingira na uwezo wa kitaasisi unaohitajika kuendelea faida katika kipindi fulani. Katika muktadha wa MKMEUWAWA uendeleu wa vijenzi vyote vya mfumo na jinsi vinavyoingiliana katika mfumo ili kutoa huduma endelevu zenye ubora kwa kundi lengwa zinaohitajika kuchunguzwa. Utaasisishaji wa mabadiliko utachangia katika uendeleu na swali kuu la utafiti kuangalia kama mfumo uko tayari kwa ajili ya upanuzi.



4.2.3 Kufanya upitiaji wa upande wa mahitaji ya huduma.

Muundo mpya wa mfumo wa EUWAWA utajikita katika mawanda na muktadha uliokubaliwa wa mfumo wa EUWAWA kama ilivyoamuliwa na wabia wa MKMEUWAWA na kama ulivyoandikwa katika mkabala wa kimwitikio wa mfumo wa EUWAWA katika awamu ya tatu. Majaribio ya mfumo mpya katika awamu ya nne, kwa hiyo yatajikita katika mawanda na muktadha tu. Inaweza kujumuisha huduma changamani zikiwemo kisomo cha watu wazima, mafunzo ya ujuzi nje ya mfumo rasmi, stadi za biashara, elimu ya masuala ya fedha, n.k. Upitiaji mwishoni mwa awamu ya nne utajikita zaidi katika kufanya majaribio ya mfumo lakini uzingatie mawanda na muktadha ujao wa mfumo wa EUWAWA nchini ambao utakuwa mpana na muundo wa upitiaji lazima ujumuishe maswali kuhusu makundi lengwa na huduma ambazo zilikuwepo kwenye majaribio. Hii itasaidia kuhakikisha iwapo mawanda na muktadha wa mfumo wa EUWAWA bado una umuhimu.

Je, upitiaji wa upande wa mahitaji una masilahi gani?

Upitiaji kwa upande wa mahitaji ya utoaji huduma za EUWAWA unavutiwa na yafuatayo:

- Kiwango ambacho huduma zimefikia makundi lengwa yaliyobainishwa yakiwa na ubora unaohitajika, ufikiwaji, uthabiti na upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika.
- Kiwango ambacho huduma zilitumiwa na kundi lengwa.
- Kiwango ambacho huduma hizi zimeleta mabadiliko katika maisha ya kundi lengwa.
- Aina nyingine za huduma ambazo kundi lengwa linaweza kuzifurahia.
- Makundi mengine lengwa ambayo majaribio ya kinfumo hayajawafikia.

Timu ya upitiaji ina jukumu la kuandaa maswali ya kina ya utafiti na madodoso ili kushughulikia mada hizi.



Je, ni vyanzo gani vya data / taarifa vitakavyojibu maswali ya utafiti?

Taarifa za upili.

Wabia wa MKMEUWAWA watakuwa wamefanya tathmini ya mahitaji katika awamu ya pili (kama wasingekuwa na taarifa zilizopatikana tayari). Tathmini ya mahitaji inachunguza mitazamo ya kundi lengwa wa EUWAWA kuhusiana na huduma za EUWAWA zilizopo pamoja na huduma zingine watakazozihitaji. Lazima pia izingatie watumiaji wapya muhimu ambao hawakujumuishwa katika progamu na miradi iliyopo ya wadau na nini mahitaji/masilahi yao yatakavyokuwa. Wasifu wa watumiaji wa sasa na muhimu wa huduma za EUWAWA unatakiwa kuwekwa kwenye maandishi kwa ajili ya miktadha ya mjini na vijijini. Ripoti ya tathmini ya mahitaji itasaidia kama utafiti wa msingi na chanzo kikuu cha taarifa kwa ajili ya upitiaji.

Wakati wa kufanya majaribio ya mfumo mpya, wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kutumia zana kama vile kadi za alama kuchunguza mtazamo wa kundi lengwa kuhusiana na huduma. Kadi za alama zinatoa chanzo zaidi cha taarifa ili kujibu maswali ya utafiti ya upitiaji kwa upande wa mahitaji na pia inaweza kuchambuliwa ili kuangalia umuhimu wa huduma zinazotolewa.

Mfumo wa U&T ambao ulitumika wakati wa kufanya majaribio ya mfumo utatoa data na taarifa, ni kwa kiwango gani kundi lengwa linatumia huduma zinazotolewa, kwa mfano:

- Viwango vya mahudhurio ya masomo, mafunzo ya stadi na aina zingine za mafunzo zinazotolewa.
- Kiwango cha wahitimu na wanaoacha masomo (mdondoko).
- Matumizi ya stadi hizi katika maisha ya kila siku ya washiriki.
- Kama kundi lengwa limeweza kuboresha maisha, na kuendelea na fursa za elimu ya juu, n.k.

Ripoti kutoka kwa wawezeshaji na wataalamu wa kiufundi kutoka katika majaribio zitakuwa zimehifadhiwa katika MUT na zinapaswa kupatikana kwa timu ya upitiaji. Aina yoyote ya upitiaji, tathmini, tafiti za uchanganuzi kifani au za chunguzi zilizofanyika katika awamu ya nne pia zipatikane.

Taarifa msingi.

Taarifa zilizopo za upili zitatoa taarifa nyingi kuhusiana na kundi lengwa na watumiaji wa huduma za EUWAWA, lakini timu ya upitiaji inapaswa pia kukusanya taarifa msingi ili kupata taarifa zilizosasisiwa kuhusu kundi lengwa. Muundo bunifu wa upitiaji unaweza kuwa na muundo unaofafana na tathmini ya mahitaji iliyofanyika katika awamu ya pili ukiunganishwa na mbinu ya kadi za alama na zana nyingine shirikishi ambazo zitawezesha mawasiliano na kundi lengwa, kama vile mbinu ya majadiliano ya vikundi na mahojiano ya mtu mmojammoja.

Je upitiaji unaweza ukafanyikaje?

Timu ya upitiaji inaweza kufanya utafiti wa kina wa mezani kwa kutumia taarifa za upili zilizopo, pamoja na ukusanyaji wa taarifa za msingi. Mawanda na uchukuaji sampuli ya ukusanyaji wa taarifa msingi vategemea upatikanaji wa fedha na muda. Ukusanyaji wa taarifa msingi zilizosasisiwa ni muhimu kusaidia aina ya maboresho kwa huduma ambazo mfumo utakapopanuliwa utazitoa. Umuhimu wa huduma kwa mahitaji ya kundi lengwa utakuwa ndiyo kichocheo kikuu cha kuamua mfumo uliopanuliwa utakavyoonekana. Iwapo muda na fedha vitakuwa havitoshi wabia wa MKMEUWAWA watafanya upitiaji taarifa kadhaa (tathmini ya ndani) kwa kutumia mbinu shirikishi za tathmini vijijini pamoja na mbinu ya majadiliano ya vikundi. Hii inatoa fursa ya kukusanya taarifa nyingi muhimu ndani ya muda mfupi ambazo zinaweza kuchangamanishwa na taarifa za upili na kushirikishana matokeo miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA kwa jili ya kuchangamanisha na kuhalalisha matokeo hayo. Zana zilizogusiwa katika awamu zilizopita zinaweza kutumika tena. Kama vile kadi za alama (awamu ya nne, sehemu ya nne) na upangaji wa viwango vya huduma za EUWAWA (awamu ya tatu, sehemu ya 4.1).

4.2.4 Kufanya upitiaji wa upande wa utoaji huduma za EUWAWA

Kufanya upitiaji wa upande wa watoa huduma na utoaji huduma wa mfumo EUWAWA kunamaanisha kupitia vipengele na vijenzi vyote vya mfumo wa EUWAWA katika dhana mkabala wa MKMEUWAWA na namna zilivyofanya kazi kama mfumo wakati wa majaribio ya awali. Matokeo ya majaribio ya mfumo huu katika awamu ya nne yatakuwa ndiyo kiini cha upitiaji.

Ni upitiaji gani ambao watoa huduma wana maslahi nao?

Upitiaji ambao watoa huduma wana maslahi nao ni:

- Maelezo yaliyohuishwa kuhusu hali ya mfumo:
 - Je, vijenzi vyote vya mfumo vipo?
 - Ni kwa kiwango gani vijenzi vya mfumo vinafanya kazi?
 - Ni kwa kiwango gani vijenzi vya mfumo vinafanya kazi kwa pamoja kama mfumo mzima?
- Alama zilizohuishwa za vijenzi, vipengele vyote vya mfumo na mfumo mzima kwa jumla.
- Kama vizuizi vya mfumo na changamoto zake vimebainishwa katika sehemu ya pili ya awamu ya pili (uchunguzi) vimefanyiwa kazi ipasavyo.
- Ulinganishaji wa hali ya uhuishaji na upimaji wa utafiti wa msingi.
- Kama muundo wa mwitikio wa mfumo wa EUWAWA umetafsiriwa katika mpango wa ufanyaji kazi kwa vitendo katika awamu ya nne.
- Kama malengo ya mipango ya miradi na muundo wa usimamizi wa programu vimefikwa wakati wa majaribio na ni kwa kiwango gani?
- Je, vihatarishi, masomo ya kujifunza, namna gani bora ya ufanyaji kazi vilivyobainishwa wakati wa majaribio?

Ni vyanzo gani vya taarifa vinavyojibu maswali ya utafiti?

Taarifa za upili

Vyanzo vya taarifa za upili katika kujibu maswali ya utafiti na kwa ajili ya uchambuzi wa baadaye ni:

- Upimaji wa mfumo wa EUWAWA ambao umefanyika na upitiaji taarifa wakati wa awamu ya pili, maelezo kuhusu hali ya kila kipengele na kijenzi cha mfumo pamoja na alama za mfumo.
- Taarifa ya warsha za uchunguzi ambazo zinabainisha chanzo kinachosababisha vizuizi katika mfumo.
- Muundo wa mkabala wa mwitikio wa EUWAWA kutoka awamu ya Tatu ambao unaonesha muundo wa mfumo mpya ulioboreshwa kwa ajili ya kufanyiwa majaribio.
- Mpango kazi kwa ajili ya kufanyiwa majaribio katika awamu ya nne ikiwa katika mipango ya miradi na muundo wa usimamizi wa programu.
- Ripoti na taarifa zilizotokana na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na kuhifadhiwa kwenye MUT. Hizi zitajumuisha ripoti kutoka kwenye taasisi wabia inayohusika na utekelezaji wa majaribio mbalimbali wakati wa Awamu ya Nne, pamoja na taarifa za kumbukumbu za warsha na mikutano iliyofanywa na wabia wa MKMEUWAWA.
- Taarifa za tathmini au upitiaji wa aina yoyote, uchanganuzi kifani, n.k. ambavyo vinaweza kuwa vimefanyika wakati wa awamu ya majaribio.



Taarifa msingi

Inashauriwa kuwa wadau wa MKMEUWAWA wanawekeza katika mfumo wa upimaji kwa kina, kwa namna moja kama ilivyotekelezwa wakati wa awamu ya pili. Wadau wanaweza kutumia tena upitiaji taalimu lakini pia wanaweza kuleta wataalamu washauri kutoka nje ya taasisi ili kupata mtazamo wa watu wa nje kuhusu MKMEUWAWA. Upitiaji taalimu utaendelea kuwajengea uwezo wabia na hivyo kuhalalisha matokeo kuhusu hali ya sasa ya mfumo. Kumbuka kwamba, tangu awamu ya pili, watu wengi wanaofanya kazi katika taasisi wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kuwa wamebadilisha nyadhifa zao na/au taasisi na hivyo ni muhimu kujengeana tena uwezo na makubaliano.

Ni namna gani upitiaji unaweza kufanyika?

Njia na vifaa vinavyotumika katika kupima mfumo kwa upande wa utoaji huduma vimeelezwa vizuri katika kijitabu cha awamu ya pili ya MKMEUWAWA na kinaweza kutumika hapa tena. Vilevile, kinaweza kutumika wakati wa kufanya warsha za uchunguzi katika sehemu ya pili (Awamu ya Pili) kujua chanzo cha vizuizi vya mfumo vilivyobaki na changamoto zake. Vikiunganishwa na uchambuzi wa data za upili na watu sahihi waliochaguliwa na majadaliano ya vikundi, upimaji wa mfumo utatoa data na taarifa za kutosha kwa ajili ya upitiaji.

4.2.5 Kuupitia ubia wa EUWAWA

Awamu ya Kwanza ya MKMEUWAWA inasisitiza umuhimu wa ubia na makubaliano miongoni mwa wadau katika kujenga mfumo wa EUWAWA kwa mafanikio. Inarudia kusema kuwa kujenga makubaliano si tukio la mara moja bali ni mchakato endelevu ambao unahusu awamu zote za MKMEUWAWA na ujenzi wa mfumo wa EUWAWA. Mafanikio ya kufanya majaribio ya mfumo mpya au ulioboreshwa katika awamu ya nne yanategemea namna nzuri wadau tofautitofauti waliopangwa kulingana na mahitaji ya muundo wa utawala wa utoaji huduma wa EUWAWA. Mahitaji ya ubia yataendelea kuwapo na yatakuwa na umuhimu mkubwa katika awamu ya tano wakati mfumo utakapokuwa umefikia ngazi ya kitaifa. Hivyo, upitiaji utahitajika pamoja na maswali kuhusu ubia uliotengeneza, makubaliano na ushirikiano miongoni mwa wabia.



Je, upitiaji kuhusu miundo ya ubia unauhitaji nini?

- Majukumu, wajibu na mamlaka waliyopatiwa wadau mbalimbali wa ubia na MKMEUWAWA. Haya yataelezwa katika usanifu wa mkabala wa mwitikio wa EUWAWA.
- Ubia ulioundwa na hatua za makubaliano haya, k.m. mkataba wa makubaliano ya awali, kushirikiana rasilimali, n.k.
- Namna ambavyo ubia huwekwa katika muundo wa mfumo wa utawala wa EUWAWA ndani ya taasisi zao.
- Hatua za makubaliano miongoni mwa wabia kuhusu hali na changamoto ndani ya mfumo wakati wa upimaji na wakati wa awamu za tatu na nne.
- Uchangamano mlalo na wima uliosababishwa na kufanya kazi kwa ubia.
- Uhusiano kati ya aina mbalimbali za wadau kama vile serikali, mashirika ya kiraia na vyuo vikuu.
- Njia na michakato waliyotumia wadau katika kutatua migogoro, kufanya kazi kwa pamoja na kufanya majadiliano.
- Njia zilizotumika katika kuwafanya wadau wawajibike.
- Uwezo wa kuendeleza taasisi ambao wadau wa MKMEUWAWA waliupata na namna ulivyotumika katika kuimarisha ubia na ujenzi wa mfumo.
- Umuhimu wa baadaye wa muundo wa ubia na utawala katika awamu ya tano. Kumbuka kuwa ubia unatarajiwa kuendelea zaidi ya awamu ya majaribio.


Ni vyanzo gani vya taarifa za kujibu maswali ya utafiti?

Taarifa za upili

- Usanifu wa mkabala mwitikio wa mfumo wa EUWAWA utatoa dondoo za majukumu, wajibu na mamlaka waliyopewa wabia pamoja na muundo wa utawala ambao utatumika wakati wa awamu ya majaribio.
- Muundo wa mipango ya usimamizi wa programu na miradi ambayo inajenga sehemu ya mpango kazi katika kutekeleza mfumo mpya katika awamu ya nne. Mipango hii itaonesha aina ya shughuli na kazi za kila kundi la wadau na wabia wanaohusika.
- Kumbukumbu za vikao vya upangaji na uratibu kati ya miundo mbalimbali ya wadau, kama vile makundi ya wadau wanaohusika na vipengele vya mfumo, uratibu wa mikutano kati wa wawezeshaji jamii, wataalamu, mikutano ya sekta mtambuko, n.k.
- Taarifa za warsha na mafunzo yaliyo ratibiwa na wadau kwa pamoja.
- Taarifa za shughuli za U&T zilizofanywa na wadau kwa pamoja.
- Taarifa zote zinazohusu MUT ambazo zilipatikana kupitia mfumo wa U&T wakati wa awamu ya majaribio.
- Mkataba wa makubaliano ya awali na makubaliano mengine ya ubia yaliyosaniwa.

Taarifa msingi

Taarifa msingi zinaweza kupatikana kwa kutumia muunganiko wa uhojaji wa kila mtu na majadiliano ya kivitundi ndani ya kila taasisi na makundi ya wabia, ikijumuisha kamati tendaji ya kitaifa ya MKMEUWAWA. Sehemu inayofuata inahusu zana mbalimbali kuhusu ubia na ushirikiano ambao tayari ulishafanyika hapo awali katika kijitabu cha MKMEUWAWA na unaweza kutumika kwa namna tofauti kujibu maswali ya utafiti kuhusu ubia na ujenzi wa makubaliano wakati wa ukusanyaji wa taarifa msingi.



Je, ni namna gani upitiaji utafanyika?

Mbali na mapitio yanayofanyika kwenye dawati yanayotokana na taarifa za upili na taarifa msingi zinaweza kupatikana pia kwa kutumia zana na mbinu zilizo orodheshwa hapa chini:

- Fanya uchambuzi wa wadau na linganisha taarifa za uchambuzi wa wadau zilizofanyika awamu ya kwanza kwa kutumia mchoro wa seti kama shirikishi, zana oneshi katika kuchambua umuhimu wa majukumu yaliyofanywa na wadau mbalimbali na uhusiano kati yao, ikijumuisha ya kundi lengwa la EUWAWA (Tazama awamu ya kwanza, sehemu ya nne).
- Tumia jedwali la uchangamani kuchambua uhusiano wa sekta mtambuko miongoni mwa wabia katika kufanya kazi (Tazama awamu ya pili, sehemu ya 2.4).
- Uchambuzi wa uwezo uwandani ili kuchunguza kinachoweza kile kilichowazuia wabia kuanzisha makubaliano na ushirikiano toshelevu kuhusu malengo ya mfumo wa EUWAWA (Tazama awamu ya tatu, sehemu ya sita).
- Mchoro wa visababishi na athari katika kuonesha madhara ya changamoto ndani ya ubia (Tazama Awamu ya Pili, sehemu ya 2.4).
- Jedwali la ushirikiano wa wadau na ushiriki wao (Tazama awamu ya tatu, sehemu ya sita).
- Kupima ngazi ya ushiriki wa wadau na wabia mbalimbali kulingana na jedwali la aina ya ushiriki na kubainisha sababu za ushiriki katika ngazi mbalimbali (Tazama awamu ya nne, sehemu ya 2.3).

4.2.6 Kuupitia mchakato wa MKMEUWAWA

Kufikia sasa, maelezo na taarifa zote za mchakato wa upitiaji zimejikita katika mfumo wa EUWAWA na mchakato wa utekelezaji na majaribio ya mfumo mpya uliosanifiwa upya. Hata hivyo, wadau wa MKMEUWAWA wanatakiwa kufuatilia wapi wameshafika katika safari yote ya MKMEUWAWA ili kutengeneza mwelekeo wa kwenda nao katika awamu ya tano na zaidi yake. Wakati wa awamu ya kwanza wadau walikusanya mpango wa muda mrefu wa mfumo kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa EUWAWA wenye kuonesha hatua walizopiga katika awamu zote. Mchakato wa upitiaji mwishoni mwa Awamu ya Nne ni sehemu ya muda mzuri wa kupumzika na kufanya tafakuri kuhusu safari nzima ya ujenzi wa mfumo wa EUWAWA kwa kutumia MKMEUWAWA. Baadhi ya maswali ya kujiuliza ni:

- Je, hatua muhimu katika mpango wa MKMEUWAWA zimefikwa kwa muda uliopangwa kulingana na matarajio?
- Nini kilichosaidia au kilichozuia kufikia mafanikio ya hatua muhimu?
- Je, mchakato wa ujenzi wa mfumo ulichukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa?
- Ni nini changamoto, mafanikio na mafunzo yaliyopatikana wakati wa mchakato?
- Ni namna gani mchakato wa MKMEUWAWA utakapo sogeza mbele wakati wa awamu ya tano na zaidi hapo?



4.3 Chambua na kukusanya matokeo ya upitiaji

Sehemu za 4.1 na 4.2 hapo juu zilielezea mchakato wa upitiaji na kutoa miongozo ya namna ya kusanifu na kufanya upitiaji. Kulingana na mawanda ya mfumo wa EUWAWA, ilishauriwa kuwa upitiaji ujumuishe sehemu mbalimbali za mfumo. Baada tu ya upitiaji kufanyika washauri wa kitaalamu na wadau wa MKMEUWAWA watatoa ripoti zifuatazo:

- Upane wa wahitaji wa mfumo wa EUWAWA.
- Upane wa watoa huduma wa mfumo wa EUWAWA.
- Ubia wa MKMEUWAWA.
- Safari ya MKMEUWAWA.

Ripoti hizi zote zinawakilisha sehemu kubwa ya mfumo wa EUWAWA na zinatakiwa kuchambuliwa kwa pamoja kwa ajili ya kupata mtazamo wa jumla kuhusu hali ya mfumo wa EUWAWA mwishoni mwa awamu ya nne na kama changamoto na vizuizi katika mfumo uliopita vimeshughulikiwa vya kutosha.

Kwa kuzingatia uchambuzi wa ripoti hizi, washauri wa kitaalamu na wabia wa MKMEUWAWA wanatakiwa kutoa ripoti ya mwisho ya awamu ya nne ambayo inatoa muhtasari na mapendekezo ya matokeo kwa ajili ya mfumo mzima wa EUWAWA kuhusu namna ambavyo mfumo wa majaribio unaweza kuwa kwenye kiwango cha juu na au kufanya marekebisho ya baadaye.

Uchambuzi wa ripoti zilizowasilishwa kuhusu upande wa wahitaji, mchakato wa ubia na MKMEUWAWA si kazi rahisi. Pia, ni muda wa kuhakikisha kuwa vigezo sita vya tathmini vilizingatiwa na kwamba mantiki yote ya upitiaji mwishoni mwa awamu ya nne/mwanzoni mwa awamu ya tano yameshughulikiwa. Sehemu inawaongoza washauri wa kitaalamu na wadau wa MKMEUWAWA kwa kuwasilisha mkabala msingi ambao unaweza kutumika katika mchakato. Kumbuka kuwa baadhi ya maswali chambuzi yanarudiwa katika ripoti zote kuhakikisha kuna mseto wa mbinu na uhalali wa matokeo.

Mkabala chambuzi katika kukusanya na kuunganisha upitiaji wa ripoti za mfumo wa EUWAWA.

Upitiajiwa ripoti na mchakato	Hatimaye, nini tunataka kujua kutoka katika hii ripoti	Aina ya mapendekezo yanayohitajika
Upande wa wahitajihuduma	• Je, watumiaji wa EUWAWA waliridhika na huduma za EUWAWA zilizotolewa (aina ya viwango, upatikanaji, n.k.)? • Je, njia za utoaji huduma ni fanisi na zinafanya kazi kama inavyotakiwa? • Je, kuna huduma zingine mpya zinazotakiwa kujumuishwa kama sehemu ya utoaji huduma za EUWAWA? • Je, kumewahi kuwapo vikwazo katika ushiriki? • Namna gani matakwa ya wajifunzaji yamejumuishwa? • Je, kuna kundi lengwa linalotakiwa kujumuishwa? Je, wanapendelea huduma gani? • Ni aina gani ya athari au mabadiliko ya haraka katika maisha ya kundi lengwa yanayoweza kuonwa kutokana na matumizi ya huduma za EUWAWA? Ni mabadiliko gani chanya na/au hasi yameshafanyika katika maisha ya kundi lengwa? • Unawezaje kulinganisha upimaji wa mahitaji ya sasa na upimaji wa awali/tafiti za msingi zilizofanyika Awamu ya Pili? • Ni maboresho gani ambayo yameshafanyika tangu mwanzo na ni changamoto gani zilizobaki? Uhusiano/Muhimu: Je, mfumo na huduma zinazotolewa bado zina mwitikio kwa mahitaji ya kundi lengwa navipaumbele vya wadau wa MKMEUWAWA, sera za nchi, mipango ya maendeleo ya taifa/sekta. Athari: Ni kwa kiwango gani mfumo wa utoaji huduma za EUWAWA unatoa athari chanya au hasi, zilizokusudiwa au zisizokusudiwa?	• Kama huduma bado ni muhimu kwa mahitaji/masilahi ya makundi lengwa, ni mabadiliko/maboresho gani yameshafanyika kwa ajili ya kuboresha, upatikanaji, utaratibu, n.k.? • Ni huduma gani zingine na au makundi gani lengwa ambayo yanatakiwa kujumuishwa katika mfumo wa EUWAWA? Hii inaathirije mawanda na muktadha wa EUWAWA? • Namna gani mfumo wa EUWAWA unaweza kupokea huduma za nyongeza na makundi lengwa? • Mapendekezo ya kuimarisha athari chanya na kupunguza athari hasi. • Ni zipi changamoto zilizobaki katika utoaji huduma ukilinganisha na upimaji wa mahitaji ya msingi? Nini chanzo cha mambo haya? • Nini kinatakiwa kufanyika kwa kiwango cha juu cha utoaji huduma zilizopo kwa eneo kubwa la kijiografia na makundi lengwa?

Upitiajiwa ripoti na mchakato	Hatimaye, nini tunataka kujua kutoka katika hii ripoti	Aina ya mapendekezo yanayohitajika
Upande wa utoajihuduma.	- Hali ya mfumo wa sasa ikoje ikilinganishwa na upimaji wa msingi uliofanyika wakati wa awamu ya pili? - Je, vijenzi vyote vinafanya kazi na ni kwa kiwango gani? - Ni kwa namna gani mfumo unafanya kazi katika kutoa huduma za EUWAWA katika vipengele na vijenzi vyote vya EUWAWA? - Ni kwa namna gani mfumo unafanya kazi katika sekta zote za nyanja za utawala? - Je, chanzo cha vizuizi na changamoto zake vimebainishwa na vimeshughulikiwa? Kwa kiwango gani au kwa nini havikushughulikiwa? - Ni kwa kiwango gani mkabalamwitikio wa mfumo sanifu wa EUWAWA (awamu ya tatu) umetekelezwa katika awamu ya nne? - Je, malengo yote ya mpango kazi wa awamu ya nne yamefanikiwa na ni kwa kiwango gani (mipango ya miradi vikundi na mkabala wa usimamizi wa programu za MKMEUWAWA)? - Je, kunaulinganifu wa upande wa utoaji na upande wa uhitaji? Umuhimu/Uhusiano: Nini utangamano wa mfumo wa EUWAWA na programu zingine zinazohusiana na haya katika sekta na nchi? Kazi zinazofanana kuratibiwa, zinafanyika? Ufanyaji kazi: Je, mfumo mpya sanifu wa EUWAWA unafanikiwa au unatarajiwa kutimiza malengo yake? Ufanisi? Je, mfumo mpya sanifu wa EUWAWA unafanikiwa au unategemewa kutimiza malengo yake?	Mapendekezo kuhusu: - Vijenzi vya mfumo bora. - Vijenzi duni vya mfumo na nini chanzo chake kwa ajili ya ufumbuzi? - Kufanya kazi kwa mfumo wote na uhusiano kati ya vijenzi na vipengele vya mfumo kwa nyanja za utawala. - Uchangamani miongoni mwa sekta. - Uboreshaji ufanisi wa mfumo. - Mkabala wa mwikitio wa usanifu wa mfumo wa EUWAWA: Je, bado ni wa kiwango cha juu au mfumounahitaji kusanifiwa upya ili kuendana na upande wa wahitaji? - Je, marekebisho na/au usanifu mpya unahitajika ili kuufanya mfumo kuwa wa kiwango cha juu?
Ubia wa EUWAWA	- Je, jinsi ubia ulivyoungwa wakati wa awamu ya nne (na kueleza katika mkabala mwikitio wa mfumo sanifu wa EUWAWA) unachangia katika mchakato wa kutoa huduma? - Ni hatua gani ya makubaliano iliyofikiwa miongoni mwa wadau wa MKMEUWAWA kuhusu ujenzi wa mfumo wa EUWAWA? - Je, wabia wametimiza mamlaka, majukumu na wajibu wao? - Nini changamotokubwa na mifano bora ya ubia? Umuhimu wa ndani: Nini michango na uhusiano kati ya majukumu ya wadau katika mfumo wa majaribio, na kazi za ndani, majukumu na mamlaka ya taasisi?	- Kushughulikia changamoto kwa makubaliano miongoni mwa mahusiano ya wabia na ubia. - Kuunda upya ubia kama unahitajika.
Mchakato wa MKMEUWAWA	- Je, kuna ushahidi wowote dhahiri wa ujenzi wa mfumo wa EUWAWA katika Awamu za MKMEUWAWA? Je, malengo yamefikikiwa? - Ni kwa namna gani MKMEUWAWA inasaidia wabia kujenga mfumo wa EUWAWA kipindi chote?	Ni kwa namna gani mchakato wa MKMEUWAWA utafanywa wakati wa Awamu ya Tano?

Vigezo endelevu vya tathmini ni mtambuko na vinatakiwa kupimwa kwa kuzingatia:

- Je, athari chanya kwa maisha ya makundi lengwa ni endelevu kwa kipindi chote? Ni nini mfumo wa EUWAWA unatakiwa kutoa ili kuhakikisha mabadiliko endelevu?
- Je, mfumo wa EUWAWA utafanya kazi katika mazingira endelevu na kuendelea kutoa huduma bora? Nini kinatakiwa kufanyika kuhakikisha kuwa taasisi inakuwa na mfumo endelevu katika ngazi za juu, za kati na chini?
- Ni kwa namna gani muundo na uhusiano wa ubia unaendelea kuchangia mfumo endelevu kwa upande wa wahitaji na watoa huduma?

Kujibu Mantiki na Kufanya Upitiaji


Uchambuzi na ripoti vilivyounganishwa kwa pamoja, vinatakiwa kujibu maswali yote na mantiki ya upitiaji, kwamba, je, mfumo uliofanyika majaribio wa EUWAWA ulifanya kazi vizuri ili kuongezwa katika awamu ya tano. Na ni marekebisho gani, kama yapo, yanahitajika kabla ya kuendelea nao katika ngazi ya kitaifa? Inawezekana kuwa baadhi ya marekebisho yatafanyika wakati unaendelezwa katika ngazi ya juu. Haya yataelezwa katika sehemu inayofuata ya kijitabu hiki.

5. KUFANYA MAREKEBISHO YA LAZIMA ILI KUJIANDAA KWA UPANUZI

5.1 Utangulizi wa Mchakato wa Marekebisho

Hatua kubwa inayofuata au ndogo ya awamu ya tano inajishughulisha na kufanya marekebisho ya msingi ya mfumo ili kufanya upanuzi, hasa kufikia ngazi ya kitaifa. Mapitio yatakuwa yametoa taarifa kuhusu hali ya sasa ya mfumo na kipi kinatakiwa kufanyika ili kuwa na mfumo utakaofanya kazi katika eneo kubwa na kwa ubora kuliko awamu ya nne ya majaribio. Hivyo, hatua ya marekebisho/nusu awamu itaanza kwa kukumbuka kuwa ni hatua ya mwisho. Hii inaongoza maboresho muhimu ambayo yanahitajika kufanyika, kwa maneno mengine, kufanya marekebisho kuelekea kwenye malengo, madhumuni na dira. Wadau wa MKMEUWAWA sharti wafanye uamuzi kama:

- Wako tayari kuendelea na mfumo uliofanyiwa majaribio katika ngazi ya kitaifa: au
- Wanaendelea nao katika awamu, ama kwa kuchagua kundi lengwa na maeneo ya kijiografia kwa ajili ya kufanya awamu tofautitofauti ya kuendelea na mfumo (mfano, idadi ya wilaya au mikoa kwa wakati mmoja); au
- Wanaweza kuunganisha vipengele na vijenzi vya mfumo ambavyo vilionesha matokeo mazuri wakati wa majaribio ya awamu ya nne wakati wa uchangamani wa mfumo wa EUWAWA, hivyo, ufundi zaidi unahitajika katika kuendelea na mfumo (zingatia tahadhari iliyoielezwa mwishoni mwa sehemu hii kwa ajili ya kuendelea na mfumo huu).



Inakadiriwa kuwa baada ya kujaribu mfumo wakati wa awamu ya majaribio, wadau na kundi lengwa la MKMEUWAWA wanaweza kuwa na hamu ya kuendelea na huduma za EUWAWA ili kuwafikia walengwa wengi zaidi na eneo kubwa la kijiografia. Uzoefu katika nchi za Ethiopia na Uganda umeonesha kwamba mafanikio ya programu changamani na vituo vya kujifunzia jamii vya EUWAWA ambavyo vinajishughulisha na maslahi na mahitaji ni muhimu, si kwa watumiaji wa EUWAWA peke yake, bali wadau wa serikali za mitaa na asasi za kiraia ndani ya jamii na wilaya sambamba na sehemu zilizofanyiwa majaribio. Hii inaweza kusabisha msukumo kwa jamii kuhusu mwenye wajibu katika ngazi za serikali za mitaa ambao baadaye atatoa msukumo kwa serikali za mikoa/majimbo na serikali kuu kuanza kutekeleza mchakato. Pia, inaweza ikaonesha kwamba uchangamani wa huduma za EUWAWA ambazo zilikuwa bado zinafanyiwa kazi sambamba na majaribio, zimedhoofika sana ukilinganisha na zile za majaribio, kwamba hii itahitaji hatua za haraka za mchakato wa kusonga mbele.

Hii inamaanisha kuwa wadau wa MKMEUWAWA hawana muda wa kupumzika/kufurahia huku wakisubiri mchakato wa majaribio wa mfumo wa EUWAWA ukamilike wote kabla ya kuanza hatua inayofuata. Hivyo, sehemu za mfumo zinaweza kuwa zimeanza kutumika kwa kiwango cha juu wakati wa mchakato wa majaribio. Kwa hali hii, wadau wa MKMEUWAWA lazima wahakikishe kwamba sehemu hizo zimejaribiwa barabara na zinaweza zikaunganishwa katika maboresho ya baadaye ya mfumo yanayoweza kuhitajika baada ya majaribio kukamilika.

Tukio la Kuboresha na Kupanua

Jedwali hapa chini linawakilisha matukio tofauti kuhusu matokeo ya upitiaji yatavyoonekana na namna ambavyo yatashawishi uwezekano wa kupanuka zaidi kulingana na marekebisho ambayo bado yanahitajika kufanywa. Kumbuka kuwa kuna uwezekano wa kuwa na mseto wa matokeo ya upitiaji ambayo yataathiri marekebisho yanayohitajika. Mfano wa matukio ambayo yamewasilishwa ukurasa unaofuata yanajikita zaidi katika changamoto zinazolazimu marekebisho ingawa inaweza kuwa pia namna bora ya mifano ambayo inaweza kutumiwa kama njia ya kufanya upanuzi zaidi.

Mifano ya matokeo ya upitiajiyanayowezezana	Mifano ya uboreshajiunaohitajika	Uwezekano wa kupanua
Mfumo wa majaribiohautoi aina ya huduma zinazohitajika kwa kundi lengwa.	Kutazamwa upya kwa pande zote mbili za wahitaji huduma na watoa huduma katika mfumo hii inaweza kusababisha kuundwa upya kabisa kwa mfumo ili kuleta uwiano. Upande wa wahitaji na watoa huduma wa mfumo wanahitaji utazamwe upya na wanaweza kuhitaji kusanifu upya mfumo ili uendane na mahitaji yao.	Upanuzi utacheleweshwa mpaka pale huduma sahihi ya EUWAWA na mawanda na muktadha wa mfumo utakaposhughulikiwa.
Huduma zinaendana na mahitaji ya kundi lengwa lakini zinatolewa bila mpangilio na kwa ubora hafifu.	Mapendekezo kuhusu marekebisho, maboresho na kuwapo kwa vijenzi sharti kuzingatiwe (mapendekezo ya upande wa watoa huduma).	Kutegemeana na idadi ya vijenzivinyotakiwa kuwapo/kurekebishwa, kufanya upanuzi kunaweza kufanyika kwa awamu.
Mazingira wezeshi ya mfumo hayapo/hayafanyi kazi sawasawa na hayawezi kutoa mwongozo kwa serikali za mitaa.	Upimaji wa vijenzi vinavyohitaji marekebisho madogo (matengezneo ya haraka) na vile vinavyohitaji kufanyiwa kazi kwa muda mrefu. Tafuta ufumbuzi wa muda.	Kufanya upanuzi kunaweza kuendelea, lakini lazima iwe katika awamu, kufanyike taratibu wakati changamoto za mfumo zikishughulikiwa katika ngazi ya juu.
Miundo ya kitaasisi inazuia uwezesaji wa utoaji huduma katika sekta na nyanja za utawala.	Tengeneza upya muundo wa taasisi na kufanya tena majaribio wakati unatafuta fursa za kuweka njia bora za utendaji kazi kitaasisi.	Hii inaweza kuchelewesha kufanya upanuzi kulingana na umuhimu wa vipengele vya mfumo. Kufanya upanuzi kwa awamu unaweza kuendelea iwapo marekebisho ni madogo.
Bajeti na mgawanyo wa rasilimali (mchakato wa usimamizi) bado hautoshelezi kwa ajili ya mchakato wa majaribio.	Tafuta mbinu mbalimbali za ukusanyaji rasilimali, mf. Ufadhili wa sekta mtambukona bajeti. Tafuta namna ya uboreshaji wa utendaji kazi kutoka kwa waendeshaji na watoa fedha kwa mfuatano.	Labda kama kuna mbadala wakukabiliana na changamoto, haya ni matokeo muhimu sana na yanaweza kuhitaji majaribio na utafiti zaidi kwa njia mbalimnali katika kukusanya rasilimali nyingi/fedha zaidi na/au kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.
Uwezo wa taasisi na wafanyakazi katika utoaji huduma za EUWAWA haujafikia kiwango cha kutoa huduma kwa makundi lengwa mengi zaidi.	Tafuta njia za kurudia na nguvu ya uwezesajiwa fursana kutengeneza muundo wa taasisi ambao unaweza kushughulikia masuala hayo.	Hii inaweza kuchelewesha upanuzina inatakiwa kushughulikiwa kwa muda mrefu endelevu. Kufanya upanuzi kunaweza kufanyika kwa awamu wakati unaendelea kufanya majaribio ya mipango ya kuwajengea uwezo na vijenzi vya mfumo unaohusiana nao.
Vifaa vilivyotengenezwa wakati wa awamu ya majaribiovinahitajika na vinatumiwa na wadau katika miradi na programu mbalimbali	Kurudianjia bora ndani ya muktadha uliopo wa vijenzi unaweza kuzisaidiawakati unazuia na kufanyia kazi udhaifu mwingine wa mfumo, mf. kukosekana kwa rasilimali zilizopo.	Matokeo haya na mpango wa namna bora ya kufanya kazi yanaweza kupanuliwazaidi kwa awamu mpakapale vijenzi vya mfumo saidizi vitakapokuwepo.
Wabia wa MKMEUWAWA walifanikiwa kuendeleza makubaliano na ushirikiano wakati wa awamu ya majaribio kwa mpango na utekelezaji wa pamoja.	Tumia matokeo ya upitiajiachanya na tafuta namna ya kuyatumia katika kushughulikia madhaifu ya mafumo na kuwapo mkabala bora wa kiutendaji kadili iwezekanavyo.	Hiki ni kichocheo muhimu kwa upanuzilakini kinaonekana tu kamakiwezeshi katika kusaidia awamu ya upanuzipale inapowezezana.

Kwa hiyo, marekebisho katika mfumo wa EUWAWA kabla ya kufanya upanuzi yanategemea matokeo ya upitiaji na uamuzi katika ngazi ya kufanya upanuzi (kitaifa, mkabala kiawamu), dira ya EUWAWA na viwezeshi vyake ambavyo vitasaidia kufanya upanuzi, mfano.

rasilimali toshelevu, makubaliano miongoni mwa wadau, n.k. Hatua za marekebisho zilizopangwa na zilizochukuliwa, sharti zitokane na mtazamo wa mfumo. Inaweza ikaonesha kwamba matokeo ya upitiaji yanabainisha usanifu mpya wa mfumo au sehemu za mfumo.

Kuendeleza Fikiria za Kimfumo

Michakato na zana katika awamu ya tatu ya MKMEUWAWA (uchambuzi mbadala na Usanifu) bado unaweza kuendelea kutumika ili kubaini njia mbalimbali mbadala na kusanifu upya mfumo au vijenzi mahususi wakati ikimakinika na athari za vijenzi vilivyobaki katika mfumo. Wadau wa MKMEUWAWA wanatahadharishwa kuendelea na fikira za mfumo na mitazamo ya mfumo. Siyo jambo zuri kuchukua kipengele muhimu cha mfumo kinachofanya kazi vizuri na kukiweka sehemu ya kile ambacho hakifanyi kazi na bado ukategemea kupata matokeo yanayofanana kama kilivyokuwa kinafanya kazi katika mfumo uliokuwa unafanya kazi vizuri (Tucker, 2016). Hatua na kanuni za Awamu ya Tatu katika

MKMEUWAWA vinabaki kuwa muhimu na pindi wadau wa MKMEUWAWA wanapokutana na matokeo ya upitiaji na mapengo na changamoto zilizobaki ndani ya mfumo, wanatakiwa kurudia mchakato wa kutafuta hatua za kuingilia na kusawazisha ambazo zitatatua changamoto nyingi za kimfumo. Hizi ni sehemu ndani ya mfumo ambamo mabadiliko madogo katika kijenzi kimoja yanaweza kuzalisha mabadiliko mengi katika vijenzi vingine na namna mfumo mzima unavyofanya kazi (Meadows, 1999). Inaweza kuwa ni jambo ambalo halihusiani tu na usanifu mpya bali pia utekelezaji na majaribio ya vijenzi fulani na visehemu vya mfumo tena kama michakato na zana zilizoelezewa katika kijitabu cha Awamu ya Nne. Sehemu inayofuata inaelezea mambo mbalimbali ya kuzingatia katika kurekebisha kwa upande wa kutoa/kupokea na mipangilio ya wadau wakiwa na mawazo ya upanuzi. Wanahitimisha na maelekezo kuhusu upangaji wa utekelezaji marekebisho.



5.2 Marekebisho katika utaratibu wa utoaji huduma za EUWAWA

Matokeo ya upitiaji yanatafsiriwa kwa upande wa kutoa huduma za EUWAWA. Kwa mfano, kama watumiaji wa EUWAWA wataelezea kutoridhika kwao, ubora na upatikanaji wa huduma za EUWAWA kama vile madarasa ya kisomo au mafunzo dhaifu ya ufundi yenye kuambatana na vifaa pungufu na vifaa vya kujifunzia, chanzo cha haya yote kinaweza kuwa ni upande wa utoaji.

Yanapofanyika marekebisho ya kuboresha utoaji huduma, wadau wa MKMEUWAWA, kama watoa huduma za EUWAWA wanaweza kutafuta machaguo mbalimbali na utaratibu wa kutoa huduma kwa ufanisi. Wanaweza kuzingatia:

Kuchangamanisha utoaji huduma za EUWAWA

Kuchangamanisha huduma za EUWAWA kunaweza kuleta maana zaidi katika uzoefu wa ujifunzaji kwa watumiaji wa huduma za EUWAWA kwamba wanaweza kuzitumia kuanzia mwanzoni mwa mafunzo. Pia, inafaidisha wadau wa MKMEUWAWA kwa kuwapa mawanda mapana ya kuwafikia wajifunzaji na uwezo wao katika kuonesha athari ya wanachokifanya. Huduma zinazohusiana na mafunzo ya ujuzi katika ufundi au kilimo yakiunganishwa na mafunzo ya ujuzi katika biashara na mafunzo ya mambo ya kifedha au upatikanaji wa huduma za kifedha na mikopo kama mtaji wa kuanzisha biashara. Huduma hizi zinaweza kutolewa na wadau mbalimbali wa MKMEUWAWA kutoka sekta mtambuko na nyanja za kiutawala. Kuchangamanisha huduma katika fungu kubwa kwa ajili ya wajifunzaji / watumia huduma za EUWAWA kuhitaji ushirikiano na marekebisho katika vijenzi vingi vya mfumo, mf.

- Mtaala unaweza kuhitaji marekebisho ili kutoa nafasi kwa mada na michango/vifaa mbalimbali.
- Vifaa vinaweza kutengenezwa kwa kuzingatia muundo wa vijarida vya wakufunzi, na vijitabu vya wajifunzaji.
- Upimaji wa wajifunzaji sharti ujumuishe vipengele vyote vya huduma.
- Wakufunzi wanaweza kuhitaji uwezeshaji wa ziada ili kuelewa mada mbalimbali kwa njia changamani.
- Taasisi zinaweza kurekebisha mipango na bajeti zao ili kuwa na utaratibu mpya wa utoaji huduma.
- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini sharti utambue athari zitokanazo na vipengele mbalimbali na hivyo kujumuisha viashirio hivyo.

Mchakato changamani katika sekta mtambuko na nyanja za utawala haujawahi kuwa rahisi na unaweza kuhitaji wabia wa MKMEUWAWA kupitia upya dira ya mfumo wa EUWAWA, kubangua bongo kwa namna mbalimbali kuhusu utoaji huduma changamani, kugundua njia bora ya mafunzo yaliyopatikana kutokana na majaribio ya awamu na kama inawezekana, kubainisha majukumu na wajibu wa wadau ili kujenga tena makubaliano. Vijitabu vilivyopita vinajumuisha vifaa shirikishi katika kusaidia mchakato huu, kama vile jedwali, uchangamani, uchambuzi wa wadau, jedwali la ushiriki wa wadau.



Uanzishaji na ufanyaji kazi wa Vituo vya Jamii vya Kujifunzia (VJK)

Vituo vya Jamii vya Kujifunzia ni mahali ambapo wajifunzaji wa EUWAWA wanaweza kupata huduma mbalimbali za EUWAWA katika sehemu moja karibu na mazingira wanayoishi. Vituo vya Jamii vya Kujifunzia vinaweza kuanzishwa katika majengo yaliyopo ambayo yanaweza kukarabatiwa na kuwekewa vifaa ili kutoa huduma mbalimbali za EUWAWA. Kama kuna fedha za kutosha, Vituo vya Jamii vya Kujifunzia vinaweza kujengwa. Vituo vya Jamii vya Kujifunzia vitahakikisha kuna vifaa ambapo huduma za EUWAWA zinaweza kutolewa kwa muda mrefu na zinaweza kutolewa kwa utaratibu wa taasisi inayo husika ndani ya mfumo wa EUWAWA. Wabia wa MKMEUWAWA watagawana majukumu kwa ajili ya huduma zitakazotolewa kwa kugawa wafanyakazi na rasilimali nyingine. Vituo vya Jamii vya Kujifunzia vitatoa fursa kwa wabia kupanua huduma zao kwa kundi lengwa kubwa zaidi na kujikita katika utoaji huduma bora. Hii itahitaji mfumo wa MKMEUWAWA kurekebisha na kuhakikisha kwamba:

- Sera, mikakati, na miongozo ya utekelezaji wa programu ndani ya kipengele cha mazingira wezeshi vinatambua na kuelezea vituo vya jamii vya Kujifunzia kama moja ya utaratibu muhimu wa kutoa huduma za mfumo wa EUWAWA. Bila kuviweka Vituo vya Jamii vya Kujifunzia katika kijenzi cha mazingira wezeshi, uendeleu wa miundo hii utaathiriwa.

- Vijenzi chini ya miundo ya kitaasisi vinarekebisha kupitia nyanja na sekta za kiutawala, ikijumuisha wadau wote wa MKMEUWAWA. Hii inaweza kuhitaji makubaliano rasmi kuhusu ugawaji wa wafanyakazi kwenye vituo vya Jamii vya kujifunzia lakini pia kurekebisha miundo katika ngazi ya kati na ya juu ambazo zitasaidia vituo vya jamii vya kujifunzia. Taratibu za utatibu ndani ya taasisi na kati ya serikali, vyama vya kiraia na vyuo vikihitaji uundwaji na kuvitaasisisha ili kuhakikisha kuwa kuna utaratibu endelevu.
- Michakato ya usimamizi kama vile mipango, bajeti, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini n.k. utatakiwa kuzingatia marekebisho ya utaratibu wa utoaji huduma wa ngazi za chini utakaonesha mabadiliko makubwa katika vijenzi vyote katika kipengele hiki. Itahitaji mipango na bajeti za sekta mtambuko, kusanifu upya mfumo ya ufuatiliaji na tathmini na mfumo ya usimamizi wa taarifa.
- Michakato ya kiufundi na namna huduma zinavyotolewa pamoja na mitaala, vifaa vya mafunzo, upimaji wa wajifunzaji utatakiwa kurekebisha ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora katika ngazi ambazo utoaji huduma za EUWAWA unalenga moja kwa moja watumiaji.

Ingawa marekebisho ya utaratibu wa utoaji huduma yanaweza kuwa muhimu, ni sehemu muhimu ya kuingilia katika kufanya uamuzi ili kuhakikisha kuwa mfumo wa EUWAWA unafikia malengo yake na dira ya muda mrefu. Matokeo na mapendekezo katika ripoti za upitiaji hayatakiwi kuchukuliwa kwa mtindo wa kijenzi kimoja baada ya kijenzi kingine, isipokuwa kwa kutumia fursa kufikia uamuzi wa kimkakati katika utoaji huduma za EUWAWA kama vile kubadili utaratibu na baadaye kurekebisha vijenzi vya mfumo kwa upande wa kutoa huduma ili kuwezesha utaratibu huu wa utoaji huduma.



5.3 Marekebisho Katika Ufanyaji kazi wa mfumo wa EUWAWA

Kurekebisha mfumo kwa upande wa utoaji huduma unaanza kwa kubainisha kama mfumo wa EUWAWA umeshughulikia mahitaji ya upande wa wahitaji wakati wa awamu ya majaribio. Hii itawezesha kutoa uamuzi kuhusu marekebisho ya utaratibu wa kutoa huduma na huduma zenewe kama ilivyojadiliwa katika sehemu iliyopita. Kwa kuzingatia uamuzi huo, vijenzi chini ya kila kipengele cha mfumo vinatakiwa kuzingatiwa kulingana na mapendekezo yaliyo katika ripoti ya upitiaji. Mchoro ufuatao katika sehemu ya 4.1 (ukurasa 15) katika kijitabu cha awamu ya tatu ya MKMEUWAWA (uchambuzi na usanifu mbadala) unatoa maelezo ya mchakato wa kufuata wakati wa kufanya uamuzi.

Wabia wa MKMEUWAWA hawawezi kujikita kwenye vijenzi vinavyohitaji marekebisho peke yake au ambavyo vinatakiwa kuwapo. Marekebisho ya moja ya vijenzi vya mfumo yanaweza kuchanua mahitaji ya marekebisho katika vijenzi vya mfumo uliopo na unaofanya kazi vizuri. Mifano ya marekebisho katika vipengele vya mfumo pamoja na vijenzi vyake vimeelezwa hapa chini. Hii itatofautiana kati ya nchi na nchi kulingana na matokeo na mapendekezo ya upitiaji.

Mazingira wezeshi

Nchi nyingi zina matatizo katika sera za elimu, lakini EUWAWA kama sekta ndogo, mara nyingi imekuwa ikiwakilishwa kwa kiwango cha chini katika mapana ya sera za elimu au ikichukuliwa kwa mtazamo finyu kama sera za kisomo, wakati wengine hawana sera na wanategemea mikakati katika kutekeleza programu na utoaji wa huduma. Uhalisia wa sekta mtambuko wa EUWAWA si rahisi kuuona katika ngazi ya sera. Matokeo ya upitiaji yataelezea kama sera za kissekta za sasa zinatoa mwanya kwa mawanda na muktadha wa EUWAWA na mfumo wa majaribio uliosanifiwa wakati wa Awamu ya Nne. Kama mfumo wa majaribio uliweza kushughulikia mahitaji ya watumiaji wa EUWAWA na kuanza kuonesha athari, itakuwa ni ya muhimu katika kufanikisha dira. Hii inamaanisha kuwa sera na mikakati itahitaji marekebisho pia. Sera hazifanyiwi upitiaji au hazibadilishwi mara kwa mara na zinahitaji ushawishi wa matokeo na utetezi. Wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kutumia fursa za upitiaji na ripoti zilizotolewa katika kunadi kwa mapana mabadiliko yanayohitajika katika ngazi za juu. Hii pia inahusisha miongozo ya kisheria ambayo inaweza kuhitaji michakato ya kuendelea kutangaza wakati wa upanuzi.



Mkabala wa mwitikio wa mfumo sanifu wa EUWAWA kutoka awamu ya tatu, utakuwa tayari umezingatia vijenzi vya miongozo ya kina ya utekelezaji wa programu ili kuwawezesha wabia wote wa MKMEUWAWA kutekeleza majaribio. Kulingana na matokeo ya upitiaji haya yanaweza kuhuishwa na kurekebisha kulingana na uzoefu uliopatikana wakati wa awamu za majaribio. Vijenzi, kama vile, mkabala wa vigezo, na muda wa kuwapo; kama hii iliwezekana wakati wa awamu ya majaribio, inawakilisha mafanikio makubwa ya mfumo. Hili pia litakuwa suala la kujumuisha EUWAWA katika mkabala wa vigezo uliopo kwa maana pana zaidi. Kama kijenzi hiki hakijashughulikiwa wakati wa awamu ya majaribio, kinatakiwa kijumuishwe katika mpango wa utekelezaji kwa ajili ya upanuzi.


Taratibu za Kitaasisi

Kuanzisha na kuendeleza mabadiliko ya mfumo wa ushirikishaji viongozi kutoka taasisi wabia wa MKMEUWAWA ni muhimu, hasa pale unapojaribu kufanya mabadiliko ya muda mrefu na magumu. Mikabala ya mfumo inahitaji kufanya kazi katika mipaka yote na ngazi za utawala za taasisi na katika muktadha wa EUWAWA inahitajika kufanya kazi katika sekta zote. Wakati mabadiliko yanapotaasisiwa, inakuwa ngumu kurudi nyuma kwenye 'mfumo wa zamani wa ufanyaji kazi' (OECD Public Governance and Territorial Development Directorate, 2017). Hii ina matokeo

chanya na hasi. Ni vigumu kuifanya kuwa ya kitaasisi na kuchukua mapendekezo ya mfumo mpya lakini inaonesha mchango wa utendaji kazi mzuri wa taratibu za kitaasisi unavyoweza kufanya kazi katika mfumo.

Miundo ya EUWAWA kwa kila taasisi mbia inaweza kuhitaji marekebisho kulingana na matokeo na mapendekezo ya upitiaji. Haya hayana budi kuzingatia marekebisho katika nyanja zote za utawala na namna, kwa mfano, serikali itakavyohakikisha kuwa kila nyanja ya serikali inatekeleza majukumu na wajibu wake ndani ya mfumo mkuu. Upangaji toshlevu wa rasilimali watu mahiri unaweza kuwa moja ya changamoto kubwa ndani ya mfumo wa EUWAWA na unaweza kuua kwa kuhisi kuwa unaweza kushawishi ama mfumo kupanuka au hapana. Hii inaweza kuhitaji uamuzi katika ngazi ya juu kutengeneza nafasi kwa wataalamu wa EUWAWA ndani ya miundo ya taasisi ya utekelezaji iliyopo.

Mbinu dhaifu za uzembe na uwajibikaji ni moja ya sababu kubwa za kushindwa kwa mfumo. Ikiwa mbinu zinazotumika katika kupima utendaji kazi dhidi ya kanuni na vigezo mara nyingi ni dhaifu, inaweza kuwa kwenye makaratasi lakini haiko katika vitendo, pamoja na taratibu dhaifu na kanuni hazipo au hazitekelezi ipasavyo (DEVCO B4 Education Discussion Paper, 2014). Usimamizi wa wawezeshaji na wawezeshaji wasaidizi wa EUWAWA unaweza kufanyika, lakini ripoti zimekuwa zitumika mara chache. Uwajibikaji wa vijenzi ni kigezo muhimu sana ili kubaini kama mfumo wa majaribio ulitimiza malengo yake au hapana na marekebisho yatafanyika kwa ajili ya upanuzi.



Vijenzi katika muundo wa ubia, hasa kati ya sekta za serikali na zisizo za serikali kwa kiasi fulani zimeshaelezewa katika sehemu ya 5.4 hapa chini. Inatakiwa kusesitizwa kuwa, mpaka pale miundo hii iliyopo na itakapotaasisishwa kama miundo rasmi katika mfumo wa EUWAWA, haiwezi kupanua mfumo wa EUWAWA. Serikali peke yake haiwezi kutoa huduma zote za EUWAWA zinazohitajika katika nchi. Vipengele vya mfumo wa taratibu za kitaasisi zinabeba uzito muhimu katika kubaini umuhimu wa kupanua mfumo majaribio.

Michakato ya usimamizi

Vijenzi chini ya michakato ya usimamizi ni mtambuko na vina uwezo wa kushawishi utendaji kazi wa vijenzi vingine. Mpango shirikishi, upangaji wa bajeti na rasilimali stahiki ni vijenzi vikubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majaribio wakati wa Awamu ya Nne na utabainisha kama upanuzi unawezekana na ni kwa kiwango gani. Kumbuka kuwa msisitizo umewekwa katika mpango shirikishi na mapendekezo ya upitiaji hayana budi kubainisha iwapo wadau wote wamehusishwa na namna upangaji unavyosambazwa katika nyanja mbalimbali za utawala na uhusishaji wa sekta nyingi. Marekebisho yanaweza kuhitajika katika mchakato huu na mfumo wa upangaji, n.k.

Kama awamu ya majaribio haikufanikiwa katika kupanga vijenzi vya bajeti na rasilimali kwa malengo ya muda mrefu ndani ya taasisi, inaweza kusesisha upanuzi wa mfumo wa EUWAWA.

Inaweza kumaanisha kuwa wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kuamua kuendelea na awamu ya upanuzi wakati wanaendelea kufanyia kazi ushahidi wa kushawishi kwa ajili ya ugawaji kitaifa na serikali za mitaa pamoja na kutafuta njia yenye ubunifu ya udhamini wa sekta zote na taratibu za kutoa huduma kwa ufanisi na ukamilifu. Vijenzi hivi havitakiwi kuachwa mpaka mwishoni mwa Awamu ya Nne, lakini mikakati ya utangazaji makini na ushahidi wa kushawishi lazima uendeleo wakati wa awamu ya majaribio kwa ajili ya kushawishi upatikaji wa fedha na kuhakikisha kuwa pale Awamu ya Tano inapofikiwa fedha inakuwapo angalau kwa ajili ya kuanza awamu ya upanuzi.

Ufuatiliaji na tathmini na usimamizi wa mfumo ya taarifa ya awamu ya majaribio utakuwa chini ya uangalizi wakati wa upitiaji, kwa ufanyaji kazi na usanifu wao, pamoja na kuthibitisha aina ya data na taarifa walizoweza kuipatia timu ya upitiaji. Mifumo inaweza kuhitaji marekebisho katika viashirio, namna data zilivyokusanywa, uchambuzi, uhifadhi na zilivyotumika. Uratibu na mchakato wa kuratibu unategemea miundo iliyokwishawekwa, lakini michakato yenyewe inaweza kuhitaji marekebisho, mf. Aina gani ya ajenda inatakiwa kuendelezwa na namna gani wabia wanawajibika katika kuiratibu, n.k.



Michakato ya kiufundi

Kama ilivyotajwa hapo juu, nchi nyingi zimelezea sera na mikakati ambayo inaonesha namna ambavyo sera itatolewa, lakini wanashindwa kuelewa hali halisi iliyopo na uwezo na vijenzi vinavyohitajika katika kutoa huduma. Vijenzi chini ya mchakato wa kiufundi vinajiegemeza katika kiini cha utoaji huduma na haya ndiyo makutaniko ya mfumo na watumiaji wa EUWAWA. Mkabala wa mfumo sanifu wa mwitikio wa EUWAWA umeelezea aina ya huduma zinazotolewa na mfumo na miongozo ya utekelezaji wa programu kwa ngazi ya kitaifa utakapowapa wabia wa MKMEUWAWA maelezo ya namna ya utoaji huduma utakavyofanyika.

Mtaala na mbinu za programu katika utoaji maudhui ya mtaala (mf. aro, mbinu ya Fuine ya REFLEKI, FAL, n.k.) utajaribiwa wakati wa Awamu ya Nne. Timu ya upitiaji itaonesha namna maudhui na mbinu zinavyopokelewa na wajifunzaji wa

MKMEUWAWA na namna walivyofaidika nazo katika kubadili maisha yao. Marekebisho yanaweza kufanyika kulingana na mahitaji ili kuhakikisha kuwa mtaala unaendana na wakati na njia za ufundishaji ni shirikishi na kuwawezesha vijana na watu wazima kupata programu zenye ubora. Vifaa vitakavyotumika katika kuwawezesha ujifunzaji vitarekebishwa ili kuendana na mapendekezo.

Vijenzi vya kujengea uwezo vinaweza kufanyiwa mabadiliko ya kimfumo. Hailengi tu wawezeshaji na wawezeshaji wasaidizi wa ndani, bali uwezeshaji wa mfumo mzima, ikijumuisha mameneja wa mfumo. Inaweza kuhitaji vyuo vikuu na vyuo kufikiria upya kuhusu mitaala na namna watakavyowaandaa wataalamu kuchukua majukumu mapya ya mfumo wa EUWAWA. Upanuzi unamaanisha kuwa wafanyakazi wengi watahitajika. Ni namna gani hawa wafanyakazi watapelele mafunzo na nani atawafundisha? Pia, inaweza kuhitaji namna ya kufikiria kuhusu taasisi fulani inayoweza kutoa baadhi ya mafunzo ya kuwajengea uwezo na mafunzo ya kufanya kazi kwa watoa mafunzo wa EUWAWA. Kipaumbele sharti kiwe kwa wataalamu wa sekta. Wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kufikiria pia nguvu ya mafunzo wakati wanazingatia ubora.

Upitiaji utaonesha namna ambavyo upimaji wa wajifunzaji umefanyika, matokeo yalikuwaje na kama upimaji wa wanafunzi unaonesha kuwa ni toshelevu kwa lengo la kuwafanya wanafunzi kuendelea na fursa nyingine za kimasomo. Msisitizo sharti uwekwe kwenye mahitaji ya mkabala wa vigezo na namna unavyohusiana na upimaji wa wajifunzaji, ufuatiliaji na tathmini, n.k. Wabia wa MKMEUWAWA watafanya marekebisho muhimu ili kuhakikisha kuwa kuna uhusiano kati ya vijenzi hivi vya mfumo.



5.4 Marekebisho katika ubia

Umuhimu wa uongozi katika marekebisho na uboreshaji wa mfumo wa EUWAWA umejadiliwa chini ya mabadiliko yaliyotajwa hapo juu na yanayohitajika katika kipengele cha mipangilio ya kitaasisi. Hata hivyo, uongozi pekee hautoshi. Umati muhimu wa watendaji au mtu mmojammoja miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA katika majukumu na nafasi mbalimbali, ambao wanafahamu haja ya mabadiliko na wanayo nia ya kuyafanyia kazi, ni muhimu sana kwa ajili ya kubadilisha mfumo (OECD Public Governance and Territorial Development Directorate, 2020). Kufanya marekebisho kunahusu tu mabadiliko. Hili linatorejesha kwenye umuhimu wa kujenga makubaliano miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA kama ilivyofafanuliwa katika Awamu ya Kwanza na kusesitizwa kama kiungo muhimu cha mafanikio katika awamu zote za MKMEUWAWA.

Upitiaji wa mfumo utakuwa umejumuishwa upitiaji wa ubia pia. Hili linajumuisha mipangilio ya kimuundo na kitaasisi miongoni mwa wabia, ambalo linashughulikiwa katika kipengele cha mfumo wa kitaasisi, lakini kwa namna wabia wanavyofanya kazi na kiwango cha makubaliano miongoni mwao. Kadiri awamu za MKMEUWAWA zilivyokuwa zikiendelea kwa muda fulani, makubaliano miongoni mwa wabia wanaweza kuwa yameathiriwa na masuala mbalimbali kama vile:

- Mabadiliko katika uongozi wa asasi ambazo ni sehemu ya ubia wa MKMEUWAWA.
- Mabadiliko ya wataalamu wa kiufundi ambao wana wajibu wa kutekeleza MKMEUWAWA, hasa wakati majaribio katika Awamu ya Nne.
- Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kimazingira na kijamii na changamoto katika nchi inayohusika.
- Mabadiliko katika sera na mikakati ambayo inaweza kuathiri mabadiliko katika mipango na ugawaji wa rasilimali.
- Mabadiliko katika miundo ya kitaasisi na namna ilivyopangiliwa kwa ndani.

Kuendeleza makubaliano katika hali za namna hii siyo rahisi na inahitaji nia ya dhati kutoka kwa kundi muhimu la wabia wa MKMEUWAWA ili kuendeleza dira na muundo wa mfumo wa EUWAWA wenye malengo yake wenyewe. Inahitaji unyumbufu ili kuitikia mabadiliko na kuyajumuisha katika muundo wa mwitikio wa mfumo wa EUWAWA katika mchakato wa majaribio.

Ubia bora kabisa wa MKMEUWAWA utakuwa na makubaliano ya dhati ili kusukuma marekebisho yanayohitajika ili kuufanya mfumo ufanye kazi katika ngazi ya taifa au angalau katika mawanda mapana kuliko awamu ya majaribio. Baadhi ya viashirio vya 'kujaribu' kiwango cha makubaliano na utayari wa wabia wa EUWAWA kukumbatia mabadiliko ya mfumo ni pamoja na (OECD Public Governance and Territorial Development Directorate, 2020):

- Ajenda ya ubunifu na mabadiliko ya mfumo imeota mizizi miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA.
- Wanafunzi/watumiaji wa huduma za EUWAWA wamekuwa kipaumbele katika michakato ya kufanya uamuzi.
- Dira na malengo ya mfumo wa EUWAWA vimefunika mitazamo ya asasi mojamoja.
- Kuna imani na mahitaji ya kufanya majaribio na kuyakumbatia mabadiliko ya mfumo.
- Mistari kati ya wadau kama vile serikali, asasi za kiraia na vyuo vikuu imefifishwa na matatizo yanayotatuliwa kwa kutazama kile kilicho bora zaidi kwa mfumo wa EUWAWA.

Ili kufikia kiwango cha makubaliano na uhusiano wa kiubia, utendaji bora uliobainishwa katika zoezi la upitiaji unapaswa kukumbatiwa na kutaasisishwa, wakati changamoto zinapaswa kushughulikiwa kwa kufanya kazi kama timu, utatuzi wa migogoro na kutumia zana katika vijitabu vilivyopita vya MKMEUWAWA kama vile uchambuzi wa wadau, kuanzisha majukumu na wajibu upya, kuchunguza mamlaka na kutafuta njia za kila mbia kutimiza majukumu yao katika mfumo.

Ubia unapaswa kujumuisha utambuzi wa kanuni, ratiba za asasi na miiko ya kitamaduni ya kila asasi mbia na jinsi inavyoweza kuchangia katika muundo wa ubia wa MKMEUWAWA. Marekebisho katika ubia yanaweza kujumuisha marekebisho ya muda mfupi kama vile kuainisha majukumu na wajibu, jambo ambalo linaweza kuangazia maeneo yenye migogoro na kuwafanya wabia kuyatazama upya malengo ya mfumo, lakini pia kunaweza kuwapo na marekebisho ya muda mrefu ambayo yatafanyika wakati wa kupanua mfumo, kwa mfano, kurejesha tena uaminifu, kuhakikisha uwajibikaji unafanyika, kuwajengea uwezo wadau, n.k.

5.5 Mpango wa kuyatendea kazi marekebisho katika mfumo wa EUWAWA na utoaji huduma

Hatua ya marekebisho katika Awamu ya Tano inajumuisha yafuatayo:

- Wadau wa MKMEUWAWA watapokea taarifa za upitiaji na kamati ya utendaji ya taifa ya MKMEUWAWA inapaswa kupanga warsha, mikutano na fursa za wadau kujumuika pamoja na kuidhinisha matokeo ya taarifa hizo.
- Warsha ya uchambuzi au mfululizo wa warsha hizo, zitatakiwa kwa ajili ya wabia kuchukua mapendekezo kutoka kwa timu za upitiaji kuhusu mtazamo wa kimfumo. Wabia wanapaswa kuzingatia hali ya mfumo baada ya majaribio, namna unavyolinganishwa na hali iliyobainishwa na utafiti wa msingi katika Awamu ya Pili na changamoto zipi pamoja na viziuzi vya mfumo vimebakia. Kama hayajabainishwa katika taarifa, basi uchunguzi kama ule wa Sehemu ya Pili wa awamu ya pili unapaswa kufanywa ili kutambua sababu kuu za masuala yaliyobainishwa.
- Michakato iliyoelezwa katika awamu ya tatu, inaweza kurudiwa kwa sababu wabia kwa sasa wapo katika ngazi inayofanana na ile ya kipindi cha baada ya Awamu ya Pili wakati mfumo ulipotathminiwa na sababu kuu za changamoto za mfumo zilipotambuliwa.



- Sehemu bora za kuingilia ili kushughulikia changamoto za mfumo zilizobakia zinapaswa kuchunguzwa na machaguo mbadala kupimwa moja dhidi ya lingine (Angalia kijitabu cha Awamu ya Tatu, Sehemu ya Nne).
- Athari ambazo marekebisho haya yanazo kwa kila kijenzi mahususi zinaweza pia kuathiri vijenzi vilivyopo na vinavyofanya kazi. Hivyo, athari hii inapaswa kutathminiwa, iwapo yatahitajika mabadiliko/marekebisho yanapaswa kufanywa katika vijenzi vilivyopo (Angalia kijitabu cha Awamu ya Tatu).
- Hatimaye, mibadala bora zaidi kwa majaribio inapaswa kuchaguliwa na usanifu mpya wa mfumo unapaswa kuoneshwa katika andiko la muundo mpya/uliosasishwa wa mwitikio wa mfumo wa EUWAWA kama ilivyofafanuliwa katika Awamu ya Tatu.

Kutegemeana na kiwango na idadi ya marekebisho yanayotakiwa, wadau wa MKMEUWAWA wanaweza kuamua kuingia katika awamu ya muda mfupi ambapo katika awamu hiyo marekebisho haya yatafanywa kabla ya kuanza kupanua wigo au kuanzisha upanuzi wa awamu wakati marekebisho yanafanywa. Mpango wa utendaji kama ule wa Awamu ya Nne unaweza kuandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa marekebisho kabla na/au wakati wa kupanua wigo.



6. PANUA WIGO WA MFUMO ULIOBORESHWA

6.1 Utangulizi wa mchakato wa kupanua wigo

Kupanua wigo kunafasiliwa kama ‘kuongeza, kuzidisha, kurekebisha na kudumisha sera, programu na miradi katika eneo la kijiografia na kwa muda fulani ili kufikia idadi kubwa zaidi ya watu’ (Linn, 2014). Katika muktadha wa kujenga mfumo wa EUWAWA na MKMEUWAWA hili linahusu kulifikia kundi lengwa kubwa zaidi (katika idadi na utofauti) katika eneo kubwa zaidi la kijiografia (ikiwezekana nchi nzima) kuliko wakati wa awamu ya majaribio. Pia, zingatia kwamba, mfumo wa kawaida uliopo wa EUWAWA ambao ulikuwa ukifanya kazi sambamba na mfumo wa majaribio inawezekana haukuwa na uwezo wa kuifikia nchi nzima na wanafunzi wote kama inavyotakiwa. Tathmini ya mfumo katika Awamu ya Pili inakuwa imebainisha sababu kwa nini hali ilikuwa hivi. Moja ya sababu inaweza kuwa ukosefu wa ushirikiano uliotaasisishwa miongoni mwa wadau wa EUWAWA. Hili mara nyingi linadhihirishwa na serikali kutekeleza programu za kiwango kikubwa za ubora duni (kwa sababu nyingi) na asasi za kiraia hutekeleza miradi ya kiwango kidogo ambayo inaweza kuonesha matokeo na athari nzuri lakini siyo lazima iwe imeandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya kuipanua baadaye.

Sehemu iliyopita kuhusu marekebisho ambayo yanapaswa kufanywa kwa ajili ya kupanua wigo pia ilibainisha kwamba, wabia wa MKMEUWAWA huenda wasiweze mara zote kuwa na ujasiri wa kusubiri mpaka awamu ya majaribio na majaribio ikamilike lakini wanaweza kulazimika kuanza kupanua sehemu za mfumo zilizojaribiwa katika awamu ya majaribio. Mifano inaweza kujumuisha mitaala, mbinu za mafunzo na uandaaji wa zana za kujifunzia ambazo zinaweza kupanuliwa katika mfumo uliopo wa kawaida. Zingatia hadhari kwamba mara baada ya mfumo uliofanyiwa majaribio kupanuliwa athari za uamuzi huu zinapaswa kutathminiwa katika vijenzi vyote vya mfumo ili kudumisha mtazamo wa mfumo mzima. Upitiaji mwanzoni mwa Awamu ya Tano, utawafahamisha wabia ni changamoto zipi zimebaki katika mfumo na kwa kiwango gani mfumo uliojaribiwa upo tayari kupanuliwa. Kwa

msingi wa taarifa hii, wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kuamua kuwa na mchakato wa kufanya upanuzi taratibu, kwa mfano, kupanua katika maeneo fulani ya kijiografia yaliyochaguliwa na/au na makundi lengwa yaliyochaguliwa kwa muda fulani. Hii inamaanisha kwamba upanuzi unaweza kufanywa kwa kipindi cha miaka kadhaa kukiwa na mpango wa namna upanuzi utakavyofanywa. Matokeo hasi ni kwamba, yanaweza kuchukua muda mrefu zaidi kuwafikia walengwa wa EUWAWA katika nchi nzima, lakini faida ya mkabala wa upanuzi wa awamu ni kwamba, wabia watajifunza masomo njiani na bado wanaweza kufanya marekebisho katika mfumo wakati wakiendelea kuusambaza katika nchi nzima. Ushawishi wenye ushahidi utaendelea kutumika, hasa katika kuwashawishi wafanya uamuzi katika ngazi za sera na mkakati. Dira ya mfumo wa EUWAWA itaendelea kuongoza mchakato wa kupanua wigo wakati ikitathmini uendeleu na athari kadiri utekelezaji unavyoendelea. Wabia wa MKMEUWAWA watatakiwa kujikita kwenye utaasisishaji wa mfumo na kuhakikisha kwamba, wabia wote wana uwezo wa kutimiza majukumu na mamlaka yao. Vipengele na masuala muhimu yanayothiri upanuzi wa mfumo yamejadiliwa katika sehemu ya 6.2.

Njia za kupanua wigo zinaweza kuwapo kwa miaka mingi na kujumuisha mfululizo wa miradi na hatua nyingi na za miaka mingi. Mahali ambapo hili linahusika, zingatia muhimu ni kuwa na njia ya upanuzi yenye mafanikio ambayo kila hatua inayochukuliwa baadaye (au mradi) unapaswa kujengwa kimfumo kuhusu mradi uliotangulia ili kutengeneza athari mkusanyiko ambazo zitaendana na lengo na dira ya muda mrefu ya mfumo wa EUWAWA uliopanuliwa. Kila mradi unapaswa kuchangia matokeo endelevu (Linn, 2014). Muundo wa usimamizi wa programu ya MKMEUWAWA uliowasilishwa katika Awamu ya Nne, unatoa utaratibu muhimu wa kuratibu miradi hii na kuhakikisha kuwa, kuna mchakato changamani wa kujenga mfumo katika mchakato wa kupanua wigo. Mazingatio na hatua katika kupanua wigo vimeelezwa katika sehemu ya 6.3.

6.2 Masuala yanayoathiri mchakato wa kupanua wigo

Masuala mengi yanaweza kuathiri uwezo wa upanuzi wa mfumo wa EUWAWA uliofanyiwa majaribio. Baadhi ya masuala haya tayari yalishajadiliwa wakati wa hatua za upitiaji na marekebisho na yanaweza kuwa mazito sana kiasi kwamba, yanaweza kusimamisha au kupunguza mchakato wa upanuzi. Masuala hayo yanahusiana kwa karibu na ufanyaji kazi wa mfumo na vijenzi vyake vyote, lakini unajumuisha mashinikizo ambayo mfumo unawekewa kutoka upande wa mahitaji na mazingira ya nje pamoja na mienendo miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA. Masuala haya kwa asili yanaweza kuwa hasi au chanya. Kwa kuzingatia masuala haya, wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kupanga na kutekeleza mchakato bora wa kupanua mfumo.

Masuala muhimu zaidi yanayoathiri mchakato wa kupanua wigo wa mfumo ni pamoja na (Linn, 2014):

- Ubunifu na ujifunzaji: Kwa kawaida upanuzi huanza na wazo jipya, muundo au mkabala katika umbo la mradi au programu ya majaribio (Awamu ya Nne). Kwa kujifunza kutokana na uzoefu huu, kwa ufuatiliaji na tathmini, kwa michakato ya kujifunza ya ndani ya asasi (mfano, kupitia duru bora za kujifunza kama ilivyopendekezwa katika Awamu ya Nne) na aina zingine za ujifunzaji wenye ushahidi, maarifa yanatengenezwa na yanaweza kutumika kupanua majaribio kupitia upanuzi, uzidishaji na uendanishaji vikiwa na athari nyingi.

- Njia za kupanua wigo: Njia ni mfululizo wa hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa katika mchakato wa kupanua wigo. Njia inaanza na ubunifu, majaribio au utendaji unahitaji dira ya kiwango cha mwisho kinachochukuliwa kwamba, kinafaa kwa ajili ya kuchukua hatua. Pia, unahitajika mkakati kwa ajili ya kufikia kiwango hicho kupitia hatua za kati. Hii inaweza kujumuisha mradi mmojammoja ambao unaweza kusaidia kuhakikisha kwamba maendeleo yanakuwapo kuelekea lengo la mwisho. Zinaweza kuja njia nyingi tofauti kwa ajili ya kupanua hatua iliyochukuliwa yenye mafanikio. Changamoto ni kuipata njia yenye mafanikio zaidi. Sehemu ya kijitabu inayohusu kurekebisha mfumo uliofanyiwa majaribio ilianza kuchunguza njia hizi na zitafafanuliwa zaidi katika sehemu ya 6.3 hapo chini.



- Waendeshaji/wasukumaji: Kama ilivyokuwa mwanzoni mwa MKMEUWAWA katika Awamu ya Kwanza, nguvu au waendeshaji wanatakiwa ili kusukuma mbele mchakato wa upanuzi kwa kufuata njia. Hawa wanaweza kuwa:
 - Kama ilivyotajwa hapo juu, masilahi katika mafanikio ya mkabala wa majaribio yanaweza kuongeza mahitaji kutoka jamii na wilaya za jirani kuanza kufanya upanuzi mapema zaidi katika maeneo yao.
 - Viongozi wenye maono au vinara mara nyingi husukuma mbele mchakato wa upanuzi. Dira inahitajika ili kutambua kuwa upanuzi unatakiwa, unapendwa na unawezekana.
 - Vichocheo vya nje kama vile migogoro ya kisiasa na kiuchumi au mashinikizo kutoka kwa watendaji wa nje, wafadhili, AZISE au mahitaji ya jamii, yanaweza kusukuma mbele mchakato wa upanuzi. Suala la ukosefu wa ajira kwa vijana barani Afrika ni moja ya mifano inayosukuma kipengele cha mafunzo ya ujuzi nje ya mfumo rasmi katika mfumo wa EUWAWA.
 - Motisha ni muhimu kwa ajili ya kusukuma mabadiliko ya tabia za wadau na wabia kwa ajili ya kufanya upanuzi endelevu uwezekane. Hii inaweza kujumuisha zawadi, mashindano na misukumo kupitia mchakato ya kisiasa, upitiaji taalimu na tathmini mbalimbali. Ufuatiliaji na tathmini dhidi ya malengo, vigezo na viwango vya utendaji ni vipengele muhimu ili kuweka motisha na uwajibikaji. Zana ya MKMEUWAWA ya tathmini za kitakwimu ya kutoa alama katika Awamu ya Pili, tayari imethibitisha kuwapo kwa mashindano na motisha kati ya wilaya, mikoa na nchi mbalimbali kufanya vizuri zaidi katika kujenga mfumo.
- Nafasi mbalimbali: Kwa ajili ya upanuzi wenye mafanikio, vikwazo na vizuizi vya mfumo vinatakiwa kuondolewa na hali wezeshi, zinazojulikanazo pia kama 'nafasi mbalimbali', lazima zitengenezwe kwa ajili ya kuchukua hatua mbalimbali ili mfumo uweze kukua. Vizuizi hivi vya mfumo pamoja na utendaji bora vitakuwa tayari vimedhihirishwa wakati wa awamu ya upitiaji na kupendekezwa kuchukuliwa kama marekebisho. Kwa mfano, vinajumuisha miongoni mwa vingine:
 - Nafasi za kifedha: Katika MKMEUWAWA hizi zitakuwa kijenzi cha mfumo cha bajeti na mgawo wa rasilimali. Kupanua wigo hakutawezekana, isipokuwa kama rasilimali zitakusanywa ili kusaidia hatua ya kupanua wigo, na/au gharama za hatua hivyo kuchukuliwa kama nafuu na fanisi zaidi na za kutosha katika nafasi iliyopo ya kifedha. Hili linajumuisha viashirio vinavyohusiana na ufanisi na kwa hiyo, litajumuisha pia vijenzi vyote chini ya kipengele cha mfumo cha mchakato ya usimamizi.
 - Nafasi ya sera: Mfumo wa kisera na kisheria ni lazima uruhusu au urekebishwe kusaidia kupanua wigo. Hili linahusu vijenzi vyote vya mfumo katika kipengele cha mazingira wezeshi. Kama ilivyodokezwa, huenda isiwezekane kufanya marekebisho haya kabla ya kuanza mchakato wa upanuzi, lakini lazima angalau iwapo nafasi ya kutosha ndani ya vijenzi vilivyopo kwa sasa ili kuwezesha upanuzi. Halafu, marekebisho zaidi na kuviweka vijenzi mahali pake kunapaswa kuendelea wakati wa mchakato wa upanuzi.



- Nafasi na uwezo wa kitaasisi: Uwezo wa rasilimali za taasisi na asasi (wafanyakazi, uongozi, n.k.), unapaswa kuandaliwa ili kuendeleza mbele mchakato wa upanuzi. Umuhimu wa kipengele cha mfumo cha mipangilio ya kitaasisi tayari umeshatajwa kutajwa katika kijitabu pamoja na vijenzi vyote katika kuamua iwapo upanuzi unawezekana au la. (Angalia hali mbalimbali katika sehemu ya 5.1). Inagusa pia vijenzi chini ya kipengele cha mchakato ya kitaalamu vinavyohusiana na kujenga uwezo.
- Nafasi ya ubia: Wabia wanahitaji kuhamasishwa pia makubaliano yanapaswa kudumishwa ili kuunga mkono juhudi za upanuzi. Wadau muhimu (wote, wanaounga mkono mchakato wa upanuzi na wanaopinga) wanahitaji kushughulikiwa kwa kuwafikia ili kuhakikisha uungwaji mkono wa kisiasa unapatikana kwa ajili ya hatua ya kupanua wigo.
- Ufuatiliaji na tathmini: Ujifunzaji kupitia ufuatiliaji na tathmini, kushirikishana maarifa, na mafunzo ni muhimu wakati wa mchakato wa upanuzi. Maarifa kuhusu nini kinafanya kazi na kile kisichofanya kazi unapaswa kutumiwa kupitia mfumo wa U&T, kuhifadhiwa katika MUT na kutumiwa na wabia wa MKMEUWAWA wakati wa upanuzi ili kufanya marekebisho zaidi pale yanapohitajika. Haupaswi kulenga athari pekee lakini pia kutathmini masuala mbalimbali yanayochangia kuamua njia zinazoweza za upanuzi ambazo unaweza kuzitumia.

6.3 Mazingatio na hatua katika upanuzi

Wabia wa MKMEUWAWA ni lazima waamue:

- Ni kwa kiwango gani mfumo wa EUWAWA uliofanyiwa majaribio upo tayari kwa upanuzi. Hili litaamuliwa na matokeo ya upitiaji, kiwango cha marekebisho yanayohitajika na masuala yanayoathiri mchakato wa upanuzi kama yalivyojadiliwa katika sehemu ya 6.2.
- Vipi ni vipimo vya upanuzi kuhusiana na kundi lengwa na nafasi ya kijiografia? Je, vinaweza kupanuliwa mpaka ngazi ya taifa au vinapaswa kufuata mpango wa hatua kwa hatua, mkabala wa polepole wa upanuzi?
- Je, hatua na njia ni zipi za upanuzi, au kwa maneno mengine, mkakati wa upanuzi na mpango wa usambazaji ni upi?



Hatua au njia za upanuzi zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo (Linn, 2014):

Hatua ya Kwanza: Weka masharti ya upanuzi

Hatua ya kwanza inahitaji kuchagua vipimo vya upanuzi. Wakitilia dira maanani, wabia wanapaswa kufasili kipimo cha mwisho ambacho kwacho mfumo unapaswa au unaweza kueleweka, kwa kuzingatia mahitaji ya watu lengwa na muda ambao mchakato wa upanuzi unapaswa kuchukua ili kufanikisha kipimo cha mwisho kinachotakiwa. Tafiti zimeonesha kwamba, upanuzi wa programu wenye mafanikio mpaka ngazi ya taifa unaweza kuchukua kati ya miaka kumi hadi kumi na mitano au hata zaidi. Hili ni muhimu kulifahamu iwapo wabia watachagua kufuata mkabala wa upanuzi wa hatua kwa hatua.

Upanuzi unaweza kuelezwa kama usambazaji wa huduma kwa wanafunzi zaidi/watumiaji wa huduma za EUWAWA katika kila nafasi ya kijiografia au unaweza pia kutazamwa kama uzidishaji mlalo wa huduma kutoka eneo moja la kijiografia kwenda jingine, au upanuzi 'wa kiutendaji' wa huduma kwa kuongeza maeneo ya ziada ya utekelezaji. Mfano huu umetajwa wakati wa kuzungumzia upanuzi wa sehemu za mfumo (au vijenzi) ambao hufanya kazi vizuri wakati wa hatua ya marekebisho kwenye mfumo wa kawaida wa EUWAWA. Linaweza pia kuwa suala la upanuzi wima ambao unahusisha kusogea kutoka utekelezaji wa ngazi ya mtaa kwenda jimboni/mkoani hadi utekelezaji wa taifa zima, mara nyingi ukihusisha mazungumzo ya kisera na msaada wa kitaalamu ili kusaidia kupata hali ya mazingira wezeshi kwa ajili ya upanuzi wenye mafanikio katika ngazi ya taifa.

Hivyo, wabia wa MKMEUWAWA watafasili vipimo, kiwango kinachohitajika na muda uliopangwa kwa ajili ya upanuzi, wakati wakijadili masuala yote yanayoathiri mchakato wa upanuzi, kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya 6.2, hili linaweza ama kuleta hatari kwa upanuzi au kutengeneza nafasi ambamo mfumo unaweza kukua.

Upungufu wowote wa habari ambao bado uapo unapaswa kuzibwa vilevile.

Uhamasishaji na makubaliano miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA unabakia kuwa sharti muhimu la upanuzi wenye mafanikio. Upanuzi wenye mafanikio unahitaji kuanzisha na kudumisha ubia na wadau wengi. Hili linajumuisha uhalalishaji wa mabadiliko ya mfumo na uongozi wa taifa na serikali za mitaa katika nchi. Bila michakato rasmi kufuatwa ambayo itahalalisha mabadiliko ya mfumo, litabakia kuwa ni zoezi jingine la majaribio.

Hatua ya Pili: Andaa mpango wa upanuzi

Hatua inayofuata itakuwa ni wabia wa MKMEUWAWA kuandaa mpango wa upanuzi, kimsingi chini ya mwongozo na maelekezo ya kamati ya utendaji ya taifa ya MKMEUWAWA ambayo inajumuisha wabia wote wa MKMEUWAWA. Sambamba na njia ya upanuzi, programu inapaswa kutoa matokeo ya kati au kufanikisha mambo ya msingi. Hili litaruhusu mabadiliko endelevu, hasa wakati wa kufanya upanuzi kwa awamu, masomo yanaweza kukusanywa kwa ajili ya awamu inayofuata. Hili pia litachangia katika kujenga makubaliano ya wadau kuhusu njia. Kutegemeana na rasilimali kuna taratibu mbalimbali za utendaji zinazotakiwa kuchunguzwa, kwa mfano:

- Wabia wa MKMEUWAWA wanaweza kutumia rasilimali zao za fedha na watu kwa ajili ya upanuzi.
- Wabia tofautitofauti wanaweza kutimiza majukumu mbalimbali katika maeneo yao ya kijiografia na ujuzi wao wa kitaalamu.
- Kupanga upya na kuhamasisha rasilimali zinazotakiwa, n.k.

Muundo wa mwitikio wa mfumo wa EUWAWA ulioboreshwa wakati wa hatua/awamu ndogo ya marekebisho utaupatia taarifa mpango wa upanuzi. Na mpango huo wa upanuzi kwa asili yake ni wa kimkakati zaidi ukiwa na dira ya muda mrefu ikionesha awamu za upanuzi na mambo ya msingi, makundi lengwa na maeneo ya kijiografia yatakayoshughulikiwa wakati wa kila awamu, n.k. Inapaswa kurejelea vijenzi vyote vya mfumo, ikijumuisha kuwa na mfumo wa U&T wenye MUT unaofanya kazi kukusanya data na taarifa kuhusu njia hiyo na kuonesha athari ya mfumo. Hili linajumuisha tathmini ya mara kwa mara au upitiaji katika maeneo ya kimkakati katika awamu zote na mambo ya msingi. Vijenzi ambavyo havikuwa vimewekwa wakati wa awamu ya majaribio (Awamu ya Nne) au bado vinahitaji marekebisho zaidi pia vinapaswa kushughulikiwa katika mpango.

Ni muhimu sana kupanga kwa kurudi nyuma kwa kujikita kwenye upanuzi kuanzia mwanzo. Wabia wanapaswa kuanza kwa kuangalia viwango wanavyotaka kupanua, gharama za kila kimoja na maana yake kwa watoa huduma na kupanga wakiwa na jambo hili kichwani. Maswali ya kutunga katika jedwali upande wa kulia yanaweza kuwaongoza wabia wakati wa mchakato wa kufanya mipango (Linn, 2014):

Mawazo	Ni hatua ipi itakayopanuliwa? Je, yapi ni matokeo ya upitiaji wa awamu ya majaribio?
Dira	Je, kiwango cha mwisho cha upanuzi kinachofaa ni kipi? Kwa hatua hii? Ni watu, wilaya, n.k., ngapi ambazo hatimaye zinapaswa kufikiwa?
Rasilimali	Nirasilimali zipi zinazopatikana kwa ajili ya upanuzi, kwa mfano, rasilimali fedha, watu, miundombinu, n.k.?
Waendeshaji	Nini au nani ni waendeshaji ambao wanasukuma au wanatarajiwa kusukuma mbele mchakato wa upanuzi? (Viongozi wa mahali, vinara, vichochezi vya nje, motisha, n.k.).
Nafasi	Ni nafasi gani zilizopo au lazima zitengenezwe ili uchukuaji hatua uweze kukuzwa ili kufikia kiwango kinachotakiwa?
Njia	Ni njia gani ambazo zinafasili namna ya uchukuaji wa hatua katika nchi utakavyopanuliwa? Ni muda gani ambao utachukuliwa ili njia (hatua) hizo ziweze kudumu? Ni vizuizi gani vya mfumo na vihatarishi vipi vinaweza kuathiri mchakato na ni nini kinaweza kufanyika ili kukomeshamasuala haya?
Majukumu ya wabia wa MKMEUWAWA	Je, majukumu ya kamati ya utendaji ya taifa ya MKMEUWAWA, migawanyo ya wabia na wabia kwa ujumla ni yapi katika mchakato wa upanuzi?



Hatua ya Tatu: Tekeleza mpango wa upanuzi

Wakati wa mchakato wa upanuzi ni muhimu zaidi kwa wabia wa MKMEUWAWA kufikiria kuhusu:

- Kuweka kumbukumbu za mchakato, ikijumuisha masomo yaliyopatikana, kupata fursa za tafakuri na kuingiza taarifa kutoka katika MUT, kwa ajili ya uboreshaji zaidi wa mfumo.
- Fanya tathmini ya unafuu wa gharama na ufanisi wa mfumo ili kutoa taarifa na kufanya mipango kwa ajili ya awamu zijazo za upanuzi.
- Fanya uchambuzi wa mara kwa mara kuhusu mahitaji na matakwa ya watumiaji wa huduma za EUWAWA, kwa kutumia kadi za alama katika jamii na zana zinazofanana na hizo.

- Fanya uchambuzi wa mahitaji ya kitaasisi yanayotakiwa kwa ajili ya upanuzi, ikiwa ni pamoja na ubia wa MKMEUWAWA. Unaweza kuhitaji marekebisho wakati wa utekelezaji. Miundo ya utawala katika nchi kwa kiwango kikubwa ndiyo itaelekeza muundo wa upanuzi. Ushahidi unatakiwa kukusanywa unaohusu iwapo mfumo unaweza kupanuliwa ndani ya miundo iliyopo au iwapo marekebisho yanahitajika.
 - Fanya uchambuzi iwapo vijenzi katika mazingira wezeshi vinawezesha mchakato wa upanuzi.
 - Kuwa na mfumo thabiti wa U&T.
 - Endelea kuratibu shughuli zote na kufuatilia utendaji unavyofanyika katika utekelezaji.
 - Dumisha kasi ya mchakato.
- Kama ilivyotajwa, mpango wa upanuzi unaweza kuchukua sura ya waraka wa kimkakati.

Utawataka wabia kuandaa mipango na bajeti za uendeshaji, kupitia makubaliano ya ubia, n.k., ambayo ni sawa na mipango iliyopo katika Awamu ya Nne ili kuhakikisha mpango wa upanuzi unatekelezwa.



Uchanganuzi kifani wa Uganda

Uzoefu wa Uganda unatoa mfano wa namna shughuli katika Awamu ya Nne na ya Tano zinavyoweza kuunganishwa. Unaonesha ugumu katika kupitia, kurekebisha na kupanua wigo wa mfumo wa EUWAWA. Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Jamii (WKMJ) nchini Uganda inahusika na kisomo cha watu wazima na maendeleo ya jamii ilifanya uamuzi mwaka 2014 kutafuta programu mrithi ya kuchukua nafasi ya programu iliyokuwapo ya KIWAWACHEMA (Kisomo cha Watu Wazima Chenye Manufaa) ambacho ilitekelezwa nchi nzima. Utafutaji wa programu mrithi ulitokana na utambuzi kwamba:

- Programu ya KIWAWACHEMA, ilikuwa haishughulikii tena mahitaji na masilahi ya kundi lengwa la EUWAWA.
- Programu ya KIWAWACHEMA, haikuwa na fedha za kutosha ili kutekelezwa nchi nzima, ilitegemea zaidi wawezeshaji ngazi ya jamii wanajitolea.
- Baadhi ya vijenzi vya EUWAWA havikuwapo kabisa, wakati vingine havikuwa vinafanya kazi kama vinavyopaswa.
- Uganda ilihitaji mfumo thabiti zaidi wa EUWAWA, ambao unaweza kutoa huduma mbalimbali za EUWAWA.
- Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Ujuzi (WJKMU) ililazimika kufanya uchunguzi kuhusu ubia na wadau mbalimbali ili kusaidia kutoa programu mpya ya EUWAWA nchini kote.


Shirika la DVV International na WJKMU walifanya makubalino ya ubia kuelekea mwishoni mwa mwaka 2014 na kuanza uchunguzi wa pamoja kuhusu programu mrithi ya KIWAWACHEMA. DVV International waliwasilisha uzoefu wao kuhusu ujifunzaji changamani ambao msingi wake ni mkabala wa mbinu ya Paulo Freire ya REFLEKTI katika Mkoa wa Karamoja nchini Uganda, ambayo ilijumuisha kisomo cha watu wazima, mafunzo ya ujuzi wa maisha, mafunzo ya stadi za biashara, Mipango ya Akiba na Mikopo Vijijini (MAMV) na maendeleo ya jamii.



Mbinu na taratibu za mkabala na mafanikio dhahiri ya majaribio huko Karamoja yaliishawishi WJKMU kuifanyia majaribio mrithi wa KIWAWACHEMA, kwa vipengele na mbinu zilezile kama mradi wa kule Karamoja. Shughuli za kuanzisha na kuwajengea uwezo watumishi wa WJKMU katika ngazi ya taifa, wilaya na tarafa zilianza mwaka 2015 na majaribio yalianza rasmi katika wilaya tatu na tarafa sita mwaka 2016. Majaribio yaliitwa programu ya Ujifunzaji Changamani wa Jamii kwa ajili ya Kuzalisha Utajiri (UCHAJAKUU) ikiendana na Dira ya Uganda ya 2040. Katika mwaka 2018 wilaya ya nne iliongezwa pamoja na tarafa mbili zaidi na mwaka 2019, tarafa mbili zaidi ziliongezwa kwa kila moja ya wilaya tatu za mwanzo.

Majaribio yalitoa fursa WJKMU na DVV International kufanya majaribio iwapo matarajio katika upande wa mahitaji yalikuwa yamefikwa, lakini pia kuhusu namna mfumo wa sasa wa EUWAWA unaweza kushughulikia programu mpya. Wakati huo, programu ya KIWAWACHEMA iliendelea katika wilaya zingine nchini. Masomo yaliyopatikana wakati wa majaribio tayari yalionesha kwamba:

- Utofauti wa huduma zinazotolewa programu mpya ya UCHAJAKUU, haukukidhi tu matakwa ya wanafunzi, lakini mahitaji yalikuwa makubwa sana, na majaribio hayakuweza kuwahudumia wanafunzi wote waliohitaji.
- Tarafa na wilaya jirani ziliwasiliana na WJKMU na kuomba utekelezaji wa UCHAJAKUU, uanze katika wilaya zao kabla majaribio hayajaisha.
- Huduma/vipengele maalumu vya UCHAJAKUU vilifanikiwa sana kiasi kwamba miongozo na mbinu mbalimbali za huduma hizi (kwa mfano, MAMV) tayari imekwisha panuliwa zaidi ya UCHAJAKUU mpaka programu zingine ndani ya WJKMU.
- WJKMU haikuwa na fedha na watumishi wa kutosha kutekeleza majaribio ya UCHAJAKUU, achilia mbali kupanua majaribio hayo.
- Ingawa sera mpya za kisomo cha watu wazima na maendeleo ya jamii zinatoa mazingira wezeshi, hazikuwa zinaendana na utaratibu wa programu mpya na vijenzi vipya kama vile mfumo wa taifa wa sifa za kitaaluma, mfumo wa U&T na MUT wa kidijiti vilikuwa ni mahitaji ya haraka.
- Taratibu mpya kama vile Vituo vya Jamii vya Kujifunzia (VJK) zinaweza kuongezwa kama majaribio madogo katika majaribio makubwa zaidi ili kujaribisha machaguo kadhaa ya utoaji huduma kwa kuzingatia uwezekano mkubwa wa kuwafikia watu wengi zaidi.



- Kufanya tathmini mbalimbali wakati wa awamu ya majaribio kunaongeza thamani ili kuonesha iwapo majaribio yanaendelea vizuri na yana uwezekano wa kuanuliwa.
- Maeneo ya kijiografia, makundi lengwa na vipengele vilivyochaguliwa kwa ajili ya upanuzi vinaweza kuanza katika awamu ya majaribio (Awamu ya Nne ya MKMEUWAWA).

Katika kipindi cha majaribio 2016 – 2021 (miaka sita), WJKMU katika ngazi za taifa na wilaya ilifanya shughuli kadhaa na ilitumia MKMEUWAWA, kuongoza mchakato wa kujenga mfumo kwa mtazamo wa kupanua UCHAJAKUU. Vijenzi kadhaa vya mfumo tayari vimewekwa mahali pake na ushawishi thabiti na endelevu wenye ushahidi na mchakato wa utetezi wa ndani (ndani ya WJKMU) imesababisha UCHAJAKUU kujumuishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa III wa Uganda. UCHAJAKUU imetangazwa rasmi kama mrithi wa KIWAACHEMA na WJKMU imeandaa mpango wa upanuzi wa hatua kwa hatua ambao utahakikisha UCHAJAKUU unapanuliwa katika wilaya na makundi lengwa zaidi baada ya miaka kadhaa.

Ingawa baadhi ya fedha na rasilimali tayari zimepatikana, lakini hazitoshi na mchakato wa utetezi utaendelea wakati wa awamu za upanuzi katika miaka ijayo.

Uzoefu wa Uganda unaonesha umuhimu wa kuufanyia majaribio mfumo mpya, kuzifanyia majaribio taratibu mbalimbali na mikabala ya utoaji huduma kwa kuangalia zaidi upande wa utoaji huduma na kuhakikisha vijenzi vipo mahali pake na vinafanya kazi vizuri, huku wakiangalia mikakati thabiti ya utetezi na ushawishi kwa nia ya kuupanua. Pia, unaonesha umuhimu wa kufanya marekebisho mapema, katika awamu ya majaribio.



7. HITIMISHO NA HATUA ZINAZOFUATA

Kutumia miwani ya kimfumo kwa matatizo magumu ni muhimu ili kuelewa na kuchora ramani ya mienendo ya mfumo ambayo inaujengea msingi. Hii inajumuisha namna uhusiano kati ya vipengele vya mfumo unavyoathiri ufanyaji kazi wake na ni hatua gani zinaweza kusababisha matokeo bora zaidi. Fikiria za kimfumo zinatusaidia kuelewa namna mifumo ilivyoundwa na kufanya kazi, nini kilicho katikati ya sehemu mbalimbali za mfumo (vipengele na vijenzi), uhusiano wake na mapengo. Pia, inamaanisha kutafakari namna ya kuchukua hatua kwa uelewa huu kwa kubuni mapendekezo na miundo ya mifumo ambayo inaweza kufanyiwa majaribio kabla ya kupanuliwa na wapi inaweza kuwa na athari kubwa zaidi (OECD Public Governance and Territorial Development Directorate, 2017). Hili linaweza kuwa na athari zote mbili chanya na hasi, na upo wajibu mkubwa kwa wabia wa kuupitia vizuri mfumo uliojaribiwa, kufanya uamuzi makini kuhusiana na marekebisho ya muundo na hatimaye kuupanua mfumo uliosanifiwa upya. Hili linaathiri maisha ya kundi lengwa la EUWAWA, kama ilivyofafanuliwa katika dira ya mfumo.

Ingawa hiki ni kijitabu cha mwisho katika mfululizo wa MKMEUWAWA na inaweza kuonekana kama Awamu ya Tano ndiyo awamu ya mwisho, kimsingi ni mwanzo wa awamu mpya. Mara baada ya mfumo uliofanyiwa majaribio kurekebishwa na shughuli nzito na ndefu ya upanuzi kuanza, wabia wa MKMEUWAWA watalazimika kuendelea kutumia mikabala ya mfumo kama njia pekee inayoweza kuwasaidia kuwa makini,


kuuelewa mfumo wanaotumia kufanya kazi na kutekeleza mabadiliko mara moja kama inavyotakiwa kutoka pande zote za mfumo wa mahitaji na wa utoaji huduma. Shughuli ya kutoa huduma za EUWAWA ni kubwa mno kwa mdau mmoja kulitekeleza na wabia wa MKMEUWAWA watalazimika kuendelea kushirikiana, kujenga makubaliano na kutaasisisha miundo yao kwa ajili ya utoaji wa huduma za EUWAWA kwa ukamilifu. Kwa hiyo, zana na michakato katika safari ya MKMEUWAWA vitatumika kwa kurudiarudia, siyo tu katika awamu ya upanuzi, lakini pia katika safari kuelekea upanuzi kama ilivyodhihirishwa katika kijitabu hiki/Awamu ya Tano. Mchakato wa upitiaji ulitumia zana za Awamu ya Pili na mchakato wa marekebisho ulitumia zana kutoka

Awamu ya Tatu. Mchakato wa upanuzi utategemea zana na michakato iliyotumika katika Awamu ya Nne, wakati mfumo mpya ulikuwa unafanyiwa majaribio na kujaribiwa. Awamu zote hizi zimeimarishwa na zinategemea makubaliano miongoni mwa wabia wa MKMEUWAWA na utawategemea wabia na kwa vipindi fulani zana za Awamu ya Kwanza. Safari ya MKMEUWAWA huwa haiishi na upanuzi wa mfumo utahitaji hata mengi zaidi kutoka kwa wabia wa MKMEUWAWA. Kiunzi cha dhana cha MKMEUWAWA, dhana na kanuni vilivyoelezwa katika kijitabu cha kwanza, 'Utangulizi wa Mkabala na Seti ya Zana', vitabakia kuwa muundo wa marejeo kwa awamu na vijitabu vyote. Hatimaye, kufikia lengo la huduma bora kwa wanafunzi wote wa EUWAWA daima kutaifanya safari kuwa ya thamani zaidi.



Seti ya Zana ya Mkabala wa Kujenga Mfumo wa Elimu na Ujifunzaji wa Watu Wazima (MKMEUWAWA) inatambua na kurejelea istilahi za EUWAWA katika machapisho yafuatayo:

- Towards an operational definition of Lifelong Learning:
UIL Working Papers No. 1 (UNICEF Institute for Lifelong Learning, 2015).
- European Adult Learning Glossary, level 2:
Study on European Terminology in Adult Education for a common language and common understanding and monitoring of the sector.
(National Research and Development Centre for Adult Literacy and Numeracy, 2008).
- Terminology of European education and training policy:
A selection of 130 key terms (second edition)
(European Centre for the Development of Vocational Training, 2014).



DEVCO B4 Education Discussion Paper. (2014).

Education System Strengthening.
DEVCO B4.

EuropeAid Co-operation Offi

*Evaluation Methods for the European Union's External Assistance:
Guidelines for project and programme evaluation.*
Luxemburg: European Communities.


European Centre for the Development of Vocational Training. (2014).

Terminology of European education and training policy.
Luxemburg: Publications Office of the European Union.

Jonathan Crowther. (1999).

Oxford Advanced Learner's Dictionary.
Oxford: Oxford University Press.

Linn. L. C. (2014).



Meadows, D. (1999).

Leverage Points Places to Intervene in a System.

Hartland: The Sustainability Institute.

National Research and Development Centre for adult literacy and numeracy. (2008).

European Adult Learning Glossary, Level 2.

London: Institute of Education, University of London.

OECD DAC. (2019, November 20).

Better Criteria for Better Evaluation.

Retrieved from www.oecd.org/dac/evaluation: oe.cd/criteria

OECD Public Governance and Territorial Development Directorate. (2017).

Working with Change: Systems approaches to public sector challenges.

OECD.

OECD Public Governance and Territorial Development Directorate. (2020).

Working with Change: Systems approaches to public sector challenges.

Europe: OECD Observatory of Public Sector Innovation.

Tucker, M. (2016).


9 Building Blocks for a World-Class Education System.

Washington DC: The National Center on Education and the Economy.

UNESCO Institute for Lifelong Learning. (2015).

Towards an operational definition of Lifelong Learning).

Hamburg: UNESCO.



DVV International
Königswinterer Str. 552 b
53227 Bonn
Germany

Tel.: +49 (0) 228 97569-0
Fax: +49 (0) 228 97569-55
info@dvv-international.de
www.dvv-international.de

DVV International

DVV International is the Institute for International Cooperation of the Deutscher Volkshochschul-Verband e.V. (DVV), the German Adult Education Association. DVV represents the interests of the approximately 900 adult education centres (Volkshochschulen) and their state associations, the largest further education providers in Germany. As the leading professional organisation in the field of adult education and development cooperation, DVV International has committed itself to support lifelong learning for more than 50 years. DVV International provides worldwide support for the establishment and development of sustainable adult education structures and systems for youth and adult learning and education. To achieve this, DVV International co-operates with civil society, government and academic partners in more than 30 countries in Africa, Asia, Latin America and Europe. DVV International finances its work through funds from the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ), the German Federal Foreign Office, the European Union as well as other donors.

The Adult Learning and Education System Building Approach (ALESBA) is a product of DVV International that can assist countries in building sustainable Adult Learning and Education (ALE) systems that can deliver a variety of ALE services to youth and adults. The ALESBA toolkit covers the conceptual framework of the approach with guidelines and practical tools to implement the approach across five phases.

The toolkit consists of the following books:

1. Introduction to the Approach and Toolkit
2. Phase One – Consensus Building
3. Phase Two – Assessment and Diagnosis
4. Phase Three – Alternatives Analysis and Design
5. Phase Four – Implement and Test
6. Phase Five – Review, Adjust and Up-scale

For further information visit:

www.mojaafrica.net
www.dvv-international.de/en/ale-toolbox